AMBOLA

SEASON 03

PALE MASHUJAA
WANAPOLISALITI TAIFA LAO

MTUNZI: PATRICK.CK



HADITHI HII NI MALI YA MWANDISHI NA HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA KWA HIYO HAIRUHUSIWI KUCHAPISHA, AU KUITUMIA KWA NAMNA NYINGINE HADITHI HII BILA RUHUSA YA MWANDISHI.HATUA KALI ITACHUKULIWA KWA YEYOTE ATAKAYEKIUKA MASHARTI HAYA..

HADITHI HII NI YA KUBUNI HAINA MAHUSIANO NA TUKIO LOLOTE LA KWELI.

SIMULIZI NYINGINE ZA MTUNZI PATRICK.CK

SIMULIZI ZA MAPENZI

1.MISS TANZANIA
2.SERENA
3.BEFORE I DIE
4.BEYOND PAIN

SIMULIZI ZA UPELELEZI

5.PENIELA
6.QUEEN MONICA
7.THE FOOTBALL
8.I DIED TO SAVE PRESIDENT
9.KIAPO CHA JASUSI
10.KIKOSI CHA SIRI
11.SIRI
12.SCANDAL(KASHFA)
13.CAPTURE OR KILL MISSION
14.JAMII YA SIRI

MAWASILIANO
0764294499

© 2020 Masimulizi.Haki zote zimehifadhiwa

ILIPOISHIA SEHEMU ILIYOPITA

“Samahani namba ya simu unayopiga haipo.Tafadhali angalia namba kwa umakini kisha jaribu kupiga tena.Kwa msaada zaidi wasiliana na huduma kwa wateja” ndivyo aliyvojibiwa Ruby baada ya kupiga namba ile.Ruby alichoka akashusha pumzi na kumtazama Mathew.

“Jibu ni lile lile kama la mwanzo namba hii haipatikani” alisema Ruby.Mathew aliichukua simu akampigia Salma.

“Ndiyo Mathew” alisema Salma

“Salma samahani kwa kukusumbua.Lini uliwasiliana na Ambola kwa kutumia namba hii uliyonipa? Aliuliza Mathew

“Siku tatu zilizopita.”

“Ahsante sana” alijibu Mathew na kukata simu.

“Namba hii ilikuwa inatumika.Salma anadai aliwasiliana na Ambola juzi” alisema Mathew

“Nini kimetokea hadi isipatikane tena? Aliuliza Ruby

“Ni mapema kusema lakini inaonekana namba hii imekwisha ondolewa katika orodha ya namba za simu hapa nchini.”

“Kwa nini iondolewe katika orodha ya namba za simu?

“Lazima ipo sababu.Lakini tuendelee kwanza kufanya uchunguzi tutabaini kwa nini namba hii haipo” alisema Mathew

“Tunaelekea wapi sasa hivi? Aliuliza Ruby

“Kwa sasa tunaelekea nyumbani kwa Ambola” alisema Mathew

Walifuata maelekezo waliyopewa na Salma wakajikuta wamefika nyumbani kwa Ambola.Walipatwa na mshangao mkubwa kwa kile

walichokikuta mahali hapo.Gari la mizigo lilikuwa linashusha vitu vya ndani vikiingizwa katika nyumba hiyo.Ilimlazimu Mathew kushuka garini akaenda kusalimiana na kijana mmoja aliyekuwa amesimama pembeni akitoa maelekezo kwa vijana waliokuwa wanashusha mizigo.

“Karibu kaka” alisema yule jamaa halafu akamuacha Mathew akaenda kutoa maelekezo kisha akarudi kwa Mathew

“Kaka karibu.Hawa vijana inabidi uwe nao karibu

vinginevyo wanaweza wakaharibu vyombo.”

“Nimeshtuka baada ya kufika hapa na kukuta kuna shughuli inaendelea.Unahamia humu ndani? Aliuliza Mathew

“Ndiyo ninahamia”

“Aliyekuwa akiishi humu amehama?

“Hapana sifahamu.Mimi nyumba hii nimeinunua sifahamu awali nani alikuwa anakaa humu.Nililetwa hapa na dalali ambaye nilimpa kazi ya kunitafutia nyumba.”alisema yule jamaa

“Ninamdai fedha nyingi mtu aliyekuwa akiishi humu na yawezekana ameamua

kuuza nyumba kimya kimya akakimbia.Unaweza ukanisaidia mawasiliano na huyo dalali tafadhali? Aliuliza Mathew.Yule jamaa ambaye alionekana kutohitaji maneno mengi alimpatia Mathew namba ya simu ya dalali ambaye alimsaidia kupata ile nyumba wakaagana Mathew akaondoka akarejea garini.

“Mambo bado magumu” alisema Mathew akamueleza Ruby kile kilichotokea.Baada ya majadiliano mafupi Ruby akaipiga ile namba ya dalali.Simu ilipokelewa.

“Hallo habari yako kaka” alisema Ruby

“Tunamshukuru Mungu tunaendelea vizuri.” Alisema jamaa aliyepokea simu

“Samahani kaka nina shida na dalali Muddy.Ni wewe? Aliuliza Ruby

“Samahani dada yangu.Huyu dalali Muddy unamfahamu?

“Simfahamu ila nimepewa namba na mtu.Ninataka kuonana naye anisaidie kutafuta nyumba”

“Pole dada huyu dalali amefariki ghafla alfajiri ya leo”

“Amefariki? Aliuliza Ruby kwa mshangao.

“Ndiyo.Amefariki dunia alfajiri ya leo na tayari

tumekwisha mzika.Hapa tupo msibani”

“Nini sababu ya kifo chake? Alikuwa mgonjwa? Ruby aliuliza

“Kwa mujibu wa mke wake, alianza kukohoa ilipofika saa tisa usiku.Ilipofika saa kumi na moja hali ilibadilika akashindwa kupumua.Walimbeba kumpeleka hospitali lakini alifia njiani” alisema yule jamaa

“Ahsante kwa taarifa na poleni sana kwa msiba” alisema Ruby akakata simu.

Ruby alimpa Mathew taarifa ile ambayo ilizidi kuwachanganya.

“Mathew ninazidi kuingiwa na hofu kubwa.” Alisema Ruby

“Kuna swali moja ambalo tunahitaji kulitafutia jibu pia.Ambola ni nani? Aliuliza Mathew

“Kutoweka kwake ghafla kunazua maswali.Kwa nini namba yake haipo tena wakati juzi ilikuwa inapatikana? Nyuma yake imeuzwa kwa haraka sana na hajulikani alipo.Biashara yake pia imefungwa.Matukio haya yote yametokea katika kipindi

kifupi sana.Swali linarudi lile lile Ambola ni nani? Aliuliza Mathew

“Mathew sifahamu wapi pa kupata majibu ya swali hilo.” Alisema Ruby

“Usihofu Ruby.Wakati wote mwanzo huwa mgumu sana.Kwa sasa tutafute namna ya kuonana na Gavana wa benki kuu ” alisema Mathew

ENDELEA……

Gari la akina Mathew lilivuka geti na kuingia katika benki ya viwanda na biashara ijulikanayo kama Industrial

and Commercial Bank of Tanzania.

“Tumemfuata nani hapa? Aliuliza Ruby kwani Mathew hakuwa amemueleza chochote kuhusu kitu wanachokifuata pale.

“Nahitaji kumuona mtu Fulani.Nisubiri humu humu garini sintachukua muda mrefu” alisema Mathew na kushuka garini.Kama kawaida yake kila sehemu aendako lazima ahakiki kwanza usalama wake.Alizungusha macho katika eneo lile

kulikuwa shwari kabisa akapiga hatua kuelekea ndani ya benki.Hakukuwa na watu wengi ndani na mara tu alipoingia alichangamkiwa na mmoja wa wafanyakazi wa benki ile.

“Kaka Mathew karibu sana.Tunafurahi leo umetumbelea” alisema yule mfanyakazi ambaye kitambulisho alichokivaa kilionesha jina lake ni Rajabu Said.

“Ahsante sana Rajabu.Mnaendeleaje hapa? Aliuliza Mathew

“Hapa tunaendelea vizuri kabisa” alijibu Rajabu

“Nafurahi kusikia hivyo.Hapa ni nyumbani kwetu sisi wafanya biashara hivyo lazima tupite walau tuwasalimu tu.Hata hivyo nina shida na meneja Zabibu.” Alisema Mathew.

“Karibu.Meneja Zabibu yuko ofisini kwake” alijibu Rajabu na Mathew akaelekea iliko ofisi ya Zabibu huku

akiwapungia mkono kuwasalimu baadhi ya wafanyakazi waliokuwa wakiendelea kuwahudumia wateja.Aligonga mlango wa ofisi ya Zabibu na sauti toka ndani ikamruhusu kuingia ndani.Alikinyonga kitasa akaufungua mlango akaingia ndani ambako alikutana na sura yenye tabasamu ya mwanamama mmoja aliyevaa suti nzuri ya rangi ya kijivu huku nywele zake akiwa amezipunguza.Mwanamama yule alitabasamu na jino lake la dhabau likaonekana.

“Mathew Mulumbi” alisema kwa furaha huku akisimama kumkaribisha Mathew

“Hallo Zabibu.” Alisema Mathew .Zabibu alitoka katika kiti chake akasalimiana na Mathew akamkaribisha katika sofa nzuri zilizokuwemo mle ofisini.

“Karibu sana Mathew.Nimefurahi leo umetutembelea.” Alisema Zabibu

“Ninashukuru sana Zabibu.Hapa ni nyumbani

kwetu hivyo si vibaya kupita hata kama hatuhitaji huduma lakini kuwajulia hali”

“Tunashukuru sana Mathew kupita hapa.Imekuwa vyema umepita kwa sababu hivi karibuni tunatarajia kuboresha sana huduma zetu ambazo zitakuwa na manufaa makubwa hasa kwa wateja wetu wakubwa kama ninyi” alisema Zabibu

“Ninashukuru kwa taarifa.Ninaomba mara tu kutakapokuwa na taarifa yoyote mpya ya uboreshwaji

wa huduma zenu nijulishwe mara moja” alisema Mathew

“Usitie shaka kuhusu hilo.Vipi biashara inakwendaje? Aliuliza Zabibu

“Biashara nzuri.Zabibu naomba nisichukue muda wako mwingi ila kuna jambo Fulani limenileta si la kiofisi” alisema Mathew.

“Karibu Mathew.Ni jambo gani hilo? Aliuliza Zabibu

“Shida yangu ni kuonana na Gavana wa benki kuu.Nafahamu wewe naye

mnafahamiana hivyo naomba unisaidie niweze kuonana naye” alisema Mathew.Zabibu alimtazama kwa sekunde kadhaa halafu akasema.

“Niambie hunitanii Mathew Mulumbi.Huna mawasiliano na Gavana?” aliuliza Zabibu

“Kwa nini nikutanie Zabibu.Ni kweli ninahitaji sana kuonana na gavana wa benki kuu lakini sina ukaribu naye.” Alisema Mathew

“Nimeshangaa inawezekanaje mtu kama

wewe usifahamiane na gavana wa benki kuu? Wewe ni mmoja wa wawekezaji wakubwa hapa nchini unapaswa kuwa karibu na watu kama hawa.Haya niambie una shida gani na Gavana? Unataka kuanzisha benki? Aliuliza Zabibu na kumfanya Mathew aangue kicheko kikubwa.

“Ni shida binafsi” alijibu Mathew.

“Sawa nitakusaidia kukuunganisha naye.” Alisema Zabibu akainuka akaenda katika meza yake akaichukua

simu yake akafungua sehemu ya kuhifadhia majina akaitafuta namba ya Gavana akampigia.

“Mheshimiwa Gavana shikamoo” alisema Zabibu baada ya Gavana kupokea simu.

“Marahaba Zabibu.Habari yako? Aliuliza Gavana Jackson Mzumile

“Ninashukuru ninaendelea vizuri”

“Ahsante sana Zabibu.Nikusaidie nini? Aliuliza Gavana

“Mheshimiwa,kuna mtu anahitaji kuonana nawe ana shida binafsi.Ni mmoja wa wawekezaji wakubwa wazawa hapa nchini”

“Ana shida ya kiofisi au? Aliuliza Gavana

“Hapana si shida ya kiofisi.Ni mambo binafsi.” Alijibu Zabibu.Zilipita sekunde kadhaa za ukimya halafu Gavana akasema

“Sawa nitaonana naye.Kama ataweza afike nyumbani kwangu saa kumi na mbili jioni ya leo nitakuwa nimerejea.Ingekuwa ni mambo ya kiofisi ningeonana naye hapa ofisini lakini kwa kuwa ni masuala binafsi nitaonana naye nyumbani ” Alisema Gavana

“Ahsante sana Gavana.Nitamuelekeza afike nyumbani muda huo.” alijibu Zabibu na kukata simu halafu akampa Mathew majibu ya Gavana.

“Zabibu ninakushukuru sana kwa msaada huu mkubwa” alisema Mathew huku akijiandaa kusimama ili aondoke.

“Usijali Mathew.Muda wowote ukiwa na tatizo unahitaji msaada karibu sana” alisema Zabibu.Waliagana Mathew akatoka na kurejea garini alikomuacha Ruby

“Mambo yamekwendaje huko? Aliuliza Ruby

“Mambo ni mazuri.” Alijibu Mathew na kumueleza Ruby kuwa mipango

inakwenda vizuri na tayari miadi ya kuonana na Gavana ilifanikiwa.

“Mungu mkubwa.Wapi tunaelekea sasa? Aliuliza Ruby

“Wakati tunasubiri ufike muda wa kuonana na Gavana,tunakwenda nyumbani kwa Gosu Gosu pengine tunaweza kupata kitu ambacho kinaweza kutusaidia kumpata Ambola.” Alisema Mathew

“Kila unapolitaja jina la Gosu Gosu moyo wangu unashtuka sana.Mwenzetu huyu inawezekana yupo katika

mateso makali sana hivi sasa au yawezekana amekwisha uawa” alisema Ruby

“Ruby usiwe na wasiwasi Gosu Gosu hawezi kuuawa” alisema Mathew

“Una uhakika gani Mathew kuwa hawawezi kumuua? Aliuliza Ruby

“Kwa namna ninavyoliona jambo hili,Gosu Gosu hajachukuliwa kwa ajili ya kufanya tu yale mauaji.Lazima ipo sababu nyingine kubwa hivyo hawawezi kumuua.Nina uhakika huo” alisema Mathew

****

Mathew Mulumbi na Ruby walifika nyumbani kwa Gosu Gosu wakapokewa na mfanyakazi wa ndani aitwaye Tecla.Aliwakaribisha akina Mathew sebuleni na kuwakirimu vinywaji.

“Tecla kuna mtu yeyote aliyefika hapa kumuulizia Gosu Gosu? Aliuliza Mathew

“Aliyefika hapa ni mchumba wake Ambola”alijibu Tecla

“Ambola alifika hapa? Ruby alishangaa

“Ndiyo alifika hapa nikampa funguo akaingia katika chumba cha bosi.Baada ya muda alitoka akiwa na sanduku dogo akanirejeshea funguo akaondoka.Nimemzoea Ambola huja hapa mara kwa mara na wakati mwigine hulala hapa hapa” alisema Tecla

“Naomba funguo ya chumba cha Gosu Gosu” alisema Mathew.Tecla alikwenda chumbani kwake

akarejea na funguo akampa Mathew ambaye aliongozana na Ruby wakapanda ngazi kuelekea katika chumba cha Gosu Gosu kilichokuwa katika ghorofa ya tatu.Waliingia ndani ya chumba kile kikubwa,kila kitu ndani ya chumba kile kilikuwa kimetulia mahali pake.

“Ambola alikuja kufanya nini katika chumba hiki? Aliuliza Ruby

“Lazima kuna kitu muhimu alikuja kukichukua humu.” Alisema Mathew huku

akiendelea kuangaza angaza mle chumbani.Alipiga magoti akatazama chini ya kitanda akaingiza mkono akatoa fremu ya picha.Alizungusha macho ukutani halafu akasema

“Nimeingia katika chumba hiki mara nyingi.Fremu hii ilikuwa na picha ya Gosu Gosu akiwa na Ambola.Inaonekana Ambola alikuja kuchukua picha na vifaa vyake vilivyokuwamo humu ndani.Swali la kujiuliza kwa nini alichukua picha zake? Je mahusiano yake na Gosu Gosu yamefika mwisho? Au alipatwa

na hasira baada ya Gosu Gosu kuondoka bila kumuaga? Aliuliza Mathew

“Kwa maelezo aliyotupa Gosu Gosu ni kweli alindoka bila kumuaga Ambola lakini kitendo cha Ambola kufika hapa na kuchukua picha yake pamoja na vifaa vyake vingine kinaashiria kuna kitu.Ingekuwa ni hasira kwa Gosu Gosu kuondoka bila kumuaga lazima angemuuliza Tecla mahali alipo Gosu Gosu lakini hakuuliza swali hilo moja kwa moja akaingia ndani na kuchukua vitu

vyake.Inaonesha ana hofu fulani.” Alisema Ruby

“Hiki alichokifanya Ambola mara nyingi hufanywa na watu waliofanya uhalifu.Huhakikisha wameondoa kabisa picha zaO sehemu mbali mbali kwa hofu ya picha zao kutumika katika kuwatafuta.Ambola kafanya nini hadi aamue kuondoa picha zake hapa kwa Gosu Gosu? Ninakubaliana nawe kabisa kuwa ana hofu ya kitu Fulani lakini nini anakihofia? Je anafahamu kitu chochote kuhusu mipango ya mama

yake? Nauliza hivyo kutokana na mambo yaliyojitokeza ndani ya kipindi kifupi.Kwanza simu yake haipatikani tena,nyumba yake imeuzwa kwa haraka sana na mpaka sasa hajulikani alipo.Mgahawa wake umefungwa bila sababu maalum.Haya yote yametokea baada tu ya Gosu Gosu kupelekwa Arusha kufanya mauaji.Swali lingine la kujiuliza kwa nini haya yote yametokea sasa? Mathew aliuliza

“Uko sahihi Mathew huyu Ambola ana hofu ya kitu fulani

ndiyo maana anaonekana anakimbia.” Aliongeza Ruby

“Lazima tuchunguze tufahamu hofu yake nini na kwa nini anakimbia.Zaidi ya yote lazima tufahamu mahali alipo” alisema Mathew.Walitoka mle chumbani wakaondoka.

Baada ya kutoka nyumbani kwa Gosu Gosu walielekea nyumbani kwa Ruby kwa ajili ya kuchukua vitu mbali mbali ambavyo vingewasaidia

****

Saa kumi na mbili na dakika nne jioni ilimkuta Mathew Mulumbi katika geti la kuingilia nyumbani kwa Gavana wa benki kuu ya Tanzania Jackson Mzumile.Tayari walinzi walikuwa na taarifa kuhusu ujio wake.Alikaguliwa kama amebeba silaha au kitu chochote cha hatari.Walinzi walipojiridhisha kuwa hana kitu chochote cha hatari walimruhusu aelekee ndani.

“Nilifanya vizuri sana kutokutembea na bastola au silaha nyingine yoyote” aliwaza Mathew wakati akielekea katika jumba kubwa la Gavana wa benki kuu.Kulikuwa na kibao kilichoelekeza maegesho ya magari ya wageni ambako Mathew aliegesha gari,akashuka na kuelekea katika kibaraza ambako msichana mmoja mwenye tabasamu alikuwa anamsubiri.

“Karibu kaka” alisema msichana yule huku akimpa mkono Mathew kwa adabu sana

“Nashukuru.Mimi ni mgeni wa Gavana.Nimemkuta? aliuliza Mathew

“Ndiyo.Karibu ndani” alisema msichana yule akamuongoza Mathew kuelekea ndani hadi katika chumba maalum cha mapumziko cha Gavana.Mara tu alipoingia ndani ya chumba kile alikutanisha macho na Jackson Mzumile Gavana wa benki kuu akiwa ameketi katika sofa akisoma gazeti.

“Karibu sana” alisema Gavana huku akiinuka kumkaribisha mgeni wake.

“Shikamoo mzee” Mathew alimsalimu Gavana.Baada ya salamu Gavana alimuelekeza Mathew aketi .Mara tu alipoketi yule msichana aliyempokea alimfuata Mathew akapiga goti moja halafu akamuuliza kinywaji ambacho angependa kutumia.Mathew aliomba apatiwe maji ya kunywa.

“Naamini wewe ndiye mgeni niliyeambiwa na Zabibu

kwamba unahitaji kuonana nami” alianzisha mazungumzo Gavana.

“Ndiyo mzee ni mimi.Ninaitwa Mathew Mulumbi mmiliki wa Mulumbi group of companies.”Mathew alijitambulisha

“Nimefurahi sana kukufahamu ndugu Mulumbi.Inapendeza kukutana na wawekezaji wakubwa kama ninyi na sisi tupo kwa ajili ya kuhakikisha tunawasaidia ili muweze kuwekeza zaidi na kutengeneza

ajira nyingi kwa watu wetu” alisema Gavana.

“Ninashukuru mzee hasa kwa sapoti tunayoipata kutoka serikalini.” Alisema Mathew

“Ni jukumu la serikali kuwalinda wawekezaje wote hasa wazawa ili kuwafanya wawe wakubwa zaidi” alisema Gavana ambaye alikuwa na sahani iliyojaa karanga zilizokaangwa.Waliendelea na mazungumzo ya kuhusiana na biashara na uwekezaji nchini Tanzania halafu Gavana akasema

“Karibu sana ndugu Mathew.Niliambiwa una suala binafsi.Niko tayari kukusikiliza”

“Mzee ninashukuru kwa kukubali kuonana nami na kunisikiliza.Kilichonileta hapa si masuala ya kibiashara”alisema Mathew.

“Ndiyo.Karibu” alisema Gavana.

“Kuna mtu anaitwa Anganile Mwaikusa unamfahamu? Aliuliza Mathew.Gavana alionekana

kushtuka kidogo hakafu akajibu.

“Ndiyo ninamfahamu.Ni dereva wangu.”

Mathew alitoa bahasha katika mfuko wake wa koti akaifungua akatoa picha ya Anganile bandia akampatia Gavana.Alipoitazama alishtuka sana.Matone ya jasho yalionekana katika upara wake.

“Mzee,huyo mtu pichani unamfahamu? Aliuliza Mathew.Gavana hakujibu kitu

aliendelea kuitazama ile picha kwa makini sana.

“Umeitoa wapi picha hii? Aliuliza Gavana

“Huyu ndiye Anganile Mwaikusa? Aliuliza Mathew

“Umeitoa wapi picha hii? Aliuliza Gavana huku sauti yake ikiwa na kitetemeshi

“Nitakueleza kila kitu mzee lakini nahitaji kufahamu kama huyu ndiye Anganile Mwaikusa” alisema Mathew.Gavana aliiweka picha

ile mezani akainamisha kichwa.

“Hapana huyu si Anganile.” Alijibu Gavana

“Unamfahamu huyo mtu pichani? Aliuliza Mathew

“Hapana simfahamu.Ni nani huyu? Mbona anaonekana kama hana uhai?

“Mzee una uhakika mtu huyu humfahamu?

“Simfahamu kabisa.Nimeshtuka kumuona katika hali hii.Ni nani huyu? Aliuliza Gavana

“Simfahamu jina lake lakini mtu huyu alikuwa akiishi chumba namba 74 Kongwa hotel jijini Arusha.” Alisema Mathew huku akimtazama Gavana.

“Ni nani kwani huyu mtu? Kwa nini unaniuliza kama ninamfahamu? Aliuliza Gavana

“Kama nilivyosema kuwa simfahamu huyu mtu ni nani.” Alisema Mathew lakini kabla hajaendelea Gavana alimkatisha.

“Kama humfahamu kwa nini unaniletea picha kuniuliza kama ninamfahamu? Aliuliza

“Mtu huyu alikuwa anatumia jina la Anganile Mwaikusa ambaye umekiri ni dereva wako” alisema Mathew

“Ni kweli Anganile ni dereva wangu wa muda mrefu .Iweje mtu huyu atumie jina lake?alihoji Gavana

“Naomba unipe dakika mbili mzee nikueleze kwa nini nimefika hapa.Huyu mtu alikuwa anatumia laini ya simu iliyosajiliwa kwa jina la

Anganile Mwaikusa.Katika kuichunguza laini yake ya simu nimekuta namba moja tu ya simu ambayo imesajiliwa kwa jina lako mzee.Tulifanikiwa pia kupata mazungumzo uliyozungumza naye” alisema Mathew akaufungua mkoba wake akaitoa kompyuta akaiweka mezani halafu akacheza mazungumzo waliyoyapata baina ya Anganile bandia na Gavana.

“Nini hiki unakicheza? Alifoka Gavana

“Mzee haya ni mazungumzo yako na huyu mtu ambaye ninamuita Anganile bandia” alisema Mathew

“Sijawahi kufanya mazungumzo yoyote na huyo mtu wala simfahamu mtu huyu ! alifoka Gavana

“Huyu mtu pia alikuwa na kamera.Baada ya kuichunguza tulikuta picha hizi” alisema Mathew na kufungua mahali zilikohifadhiwa picha za Regina.Alimsogezea gavana

komyuta ile ili azitazame vizuri.

“Unamfahamu huyu mtu pichani? Aliuliza Mathew.Gavana alizitazama picha zile halafu akainua kichwa akamtazama Mathew.

“Who are you? Aliuliza kwa ukali

“Utanisamehe mzee kama nimekosea lakini nimekuja hapa kwako kutaka kuufahamu ukweli.Huyu mtu alizungumza nawe akakujulisha kuwa tayari amefika Arusha na ameanza

kazi.Tunaamini kazi aliyokuwa anaifanya ni hii ya kumchunguza huyu mwanamke pichani ambaye anaitwa Regina Zanga naibu katibu mkuu wa chama cha ukombozi wa Afrika.”

“Subiri kwanza kijana ! alisema Gavana kwa ukali

“Nimekusikia zaidi ya mara moja unatamka tumefanya hivi,tumegundua vile.Uko wewe na nani? Wewe na hao wenzako ni akina nani? Ni polisi? Usalama wa taifa?

Au ni akina nani? Aliuliza Gavana

“Mimi si polisi au usalama wa taifa ila nimewahi kufanya kazi katika shirika la ujasusi Tanzania.” Alisema Mathew.Gavana alimtazama kwa mshangao.Mdomo ulibaki wazi.

“Usiku wa kuamkia leo,huyu mwanamke ambaye alikuwa anafuatiliwa na huyu Anganile bandia alinusurika kuuawa.Naamini umekwisha zisikia taarifa hizo” alisema Mathew

“Huyu mwanamke anatafutwa na jeshi la polisi kwa mauaji ya kikatili aliyoyafanya huko Arusha”alisema Gavana

“Hapana hakuua mtu kama inavyodaiwa.Ameangushiwa kesi” alisema Mathew na Gavana alimtazama kwa mshangao

“Bastola yake imetumika kufanya mauaji unawezaje kumtetea kuwa hajaua mtu?

“Ni kwa sababu nilikuwepo eneo la tukio na

mimi ndiye niliyemuokoa asiuawe” alisema Mathew.Gavana alimtazama kama vile anatazamana na Kobra.

“Nimemuhoji Regina nikamuuliza kama anamfahamu yule mtu aliyekuwa anamfuatilia amekiri hamfahamu lakini anahisi ni wewe ndiye uliyemtuma yule mtu amfuatilie.Ametoa sababu unamchunguza kwa kuwa unahisi anahusika katika tukio la kupotea kwa mwanao Kelvin.Mzee nimekuja hapa

kutafuta majibu.Ni kweli unamchunguza Regina? Aliuliza Mathew.Gavana aliinamisha kichwa akawaza halafu akasema.

“Huyu mtu pichani yuko wapi kwa sasa? Unafahamu mahali alipo? Aliuliza Gavana

“He’s dead” alijibu Mathew

“Mungu wangu ! alisema Gavana kwa sauti ndogo ya mshtuko.Kilipita kimya kifupi halafu akauliza

“Who killed him?

“Siwafahamu bado ni akina nani.Ninaendelea kuwachunguza ndiyo maana nimekuja kwanza hapa kwako nikitaka kumfahamu huyu mtu ni nani” alijibu Mathew.Gavana alivuta pumzi ndefu halafu akasema.

“It’s true” alinyamaza kwa sekunde chache halafu akaendelea.

“Huyu mtu ninamfahamu.Ni kweli mimi ndiye niliyemtuma Arusha” alinyamaza tena kwa sekunde kadhaa halafu akaendelea.

“Huyu mtu jina lake halisi ni Johnson Kumbi.Ni raia wa Zambia.Kazi yake ni mpelelezi wa kujitegemea” alinyamaza tena kwa sekunde kadhaa.

“Ni mimi niliyemleta hapa nchini na kazi kubwa iliyomleta hapa nchini ni kumchunguza Regina.” Alinyamaza akavuta pumzi ndefu akajiegemeza tena sofani.

“Huyu mwanamke alikuwa na mahusiano ya kimapenzi na mwanangu Kelvin.Sikuwahi kuonana naye ila Kelvin

aliniambia atamleta kwetu mwanamke huyo kumtambulisha.Japokuwa Kelvin alikuwa na kazi yake nzuri pamoja na biashara zake kadhaa,lakini bado alikuwa akiishi hapa nyumbani.Si kwamba hakuwa na nyumba.Anayo nyumba yake kubwa na nzuri ila ni mimi ambaye nilimtaka asihamie katika nyumba hiyo na aendelee kuishi nasi hapa nyumbani.Ni kijana tuliyempenda sana.Licha ya kwamba ni mwanangu lakini alikuwa kama rafiki

yangu.Nilizoea kumwita bwana mdogo.Mara nyingi tulikuwa tukitaniana sana” alinyamaza kidogo.

“Siku kama tatu hivi kabla hajatoweka nilimwona akiwa ni mtu mwenye mawazo mengi sana.Kwa mzazi ni rahisi kujua kama mwanao ana matatizo.Nililifahamu hilo na nikamuuliza kama ana tatizo lolote alinijibu kuwa hana tatizo lolote.Nilimtumia hata mama yake amdadisi kama ana tatizo lakini aliendelea kukana kuwa hana tatizo lolote.Tuliamini yawezekana ni

masuala ya mapenzi na tukaamua kumpa muda.” Alinyamaza akatazama chini kwa sekunde chache

“Siku ya tukio nilipigiwa simu na mkuu mmoja wa kituo cha polisi ambaye ni rafiki yangu akanijulisha kuna tukio limetokea linamuhusu mwanangu.Nilikwenda haraka sana eneo la tukio na kukuta juhudi za kumsaka Kelvin zikiendelea.Nguo alizokuwa amevaa zilikutwa garini hii ina maana aliingia majini akiwa na bukta pekee.Simu yake ilikutwa garini pia na baada ya

kuangalia mawasiliao yake tuligundua mtu wa mwisho kuwasiliana naye alikuwa ni Regina.Nilimpigia simu akanielekeza anakoishi nikamfuata.Alikana kufahamu chochote kuhusu kupotea kwa Kelvin.” Alinyamaza tena.

“Jeshi la polisi lilifanya uchunguzi wake na Regina alikuwa mmoja wa waliolisaidia jeshi hilo katika uchunguzi.Baada ya miezi kadhaa ya uchunguzi jeshi la polisi walitoa taarifa kuwa Regina hahusiki na kupotea kwa Kelvin.Kama familia

tuliumizwa sana na tuliamua kumuachia Mungu.Baada ya kipindi Fulani kupita nilifuatwa na rafiki yangu anafanya kazi katika idara moja nyeti ya usalama hapa nchini akaniambia kuna kitu kuhusiana na tukio lile la kupotea kwa Kelvin.Alinitaka nifanye uchunguzi kwa siri.Alinisaidia nikampata mpelelezi wa kuchunguza suala hili.Siku mbili tu baada ya kuanza kazi hiyo alikutwa amekufa katika mtaro wa maji.Hapo ndipo nilipoanza kuamini kuwa kuna kitu katika

tukio hilo la kutoweka Kelvin.Nilitafuta mpelelezi mwingine lakini naye aliuawa baada ya wiki mbili.Huyu mpelelezi wa pili aliniambia anahisi aliyekuwa mpenzi wa Kelvin yaani Regina anahusika katika tukio lile au kuna kitu anakifahamu" alisema Gavana.

"Samahani kwa kukukatisha mzee kuna kitu nataka kufahamu.Huyu mpelelezi wa pili alikueleza Regina anahusikaje katika tukio hilo la kupotea Kelvin? Mathew aliuliza

“Hakunieleza ila katika uchunguzi wake wa awali alidai hivyo kwamba anawekeza nguvu katika kumchunguza Regina kwa sababu anahisi kuna kitu anakifahamu.Hakuimaliza kazi yake akauawa.Wapelelezi wawili kuuawa ilinishawishi niamini kupotea kwa Kelvin kuna jambo kubwa ndani yake hivyo niliamua kumtafuta mpelelezi mwingine kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kuendelea na uchunguzi.Nilimpata Johnson Kumbi kutoka Zambia.Kwa vile mpelelezi wa

pili alikwisha mtaja Regina kuwa anafahamu kitu kuhusu kupotea kwa Kelvin nilimtaka Johnson aanzie upelelezi wake kwa Regina.Kwa wakati huo Regina alikuwa jijini Arusha katika maandalizi ya kuzindua kampeni za uchaguzi mkuu.John alikuwa anazungumza Kiswahili vizuri sana na kwa vile sikutaka aonekane ni raia wa kutoka nje nilimpa laini ya simu iliyosajiliwa na dereva wangu Anganile ili aitumie katika mawasiliano.Kama ilivyokuwa kwa wengine naye pia kabla

hajafika mbali katika uchunguzi wake ameuawa.Bwana Mathew hayo ndiyo maelezo ninayoweza kukupa kuhusiana na huyu mtu.Unafahamu nani kamuua? Nina uhakika mkubwa kwamba aliyemuua Johnson ndiye aliyewaua wale wapelelezi wengine wawili na lazima wanafanya hivyo kuficha kitu Fulani kisijulikane" Alisema Gavana

"Mheshimiwa Gavana kwanza kabisa ninakupa pole nyingi kwa tukio hili la kupotea mwanao na kwa

wapelelezi wote kuuawa.Kwa sasa mimi na wenzangu tumeingia katika kazi ya kuwasaka hawa watu.Maelezo haya uliyonipa leo yatatusaidia sana katika uchunguzi wetu.Ninakuahidi mzee pale nitakapokuwa na taarifa zozote kuhusiana na hawa watu nitakujulisha.” alisema Mathew

“Ninachojiuliza hawa watu wanafahamuje mipango yangu? Walijuaje kama nimemtuma Johnson Arusha kwenda kumchuguza Regina? Aliuliza Gavana

“Mzee,huu si mpango wa mtu mmoja.Ni mtandao mkubwa tena unaowahusisha watu wazito.Wana mbinu nyingi wanazotumia.” Alijibu Mathew

“Who are they? Kitu gani wanakificha kisijulikane? Kwa nini wakataka kumuua pia Regina? Aliuliza Gavana.

“Baada ya kumuokoa Regina nilimuhoji sababu ya yeye kutaka kuuawa.Alinijibu kuwa anahisi ni chama chake ndio wanaotaka kumuua.” Alisema Mathew na sura ya

Gavana ilibadilika kidogo.Alionekana kushangaa

“Chama wanataka kumuua? Kwa nini? Aliuliza Gavana

“Kuna sababu kadhaa kwa nini anahisi wanataka kumuua.Kwanza kabisa ana mpango wa kuhama chama.Anahisi mpango wake huo wa kuhama chama umevuja ndiyo maana wanataka kumuua” alisema Mathew

“Bado sielewi.Mtu unawezaje kuuawa kwa

kuhama chama? Mbona watu wengi wanahama vyama tena wengine ni wenye nyadhifa kubwa katika vyama hivyo lakini hatujasikia wakiuawa?Kwa nini iwe kwa Regina? Aliuliza Gavana

“Kwa maelezo yake mwenyewe anadai wanataka kumuua baada ya kuzijua baadhi ya siri kubwa za chama na wanahisi kama akihama chama anaweza akazivujisha siri hizo kwa chama anachotaka kuhamia.” Alisema Mathew

“Bado hainiingii akilini.Siri ipi kubwa hadi atakiwe kuuawa? Aliuliza Gavana.

“Kwanza ni kuhusiana na mmiliki wa chama hicho” Mathew alimueleza Gavana kuhusiana na mtu anayeitwa Mfadhili wa chama.

“Baada ya Regina kugundua uwepo wa mtu huyo alinyamazishwa kwa kupewa kiasi kikubwa cha fedha na onyo kuwa akifumbua mdomo wake kusema chochote utakuwa ni mwisho

wake.Alinyamaza kimya lakini aliamua kuhama chama baada ya kugundua jambo lingine kubwa.” Mathew alinyamaza baada ya Gavana kuonekana anataka kusema kitu.

“Ni jambo gani hilo alilogundua?

“Kuna njama za kuvuruga uchaguzi mkuu” alisema Mathew.Gavana alivuta pumzi ndefu halafu kimya kifupi kikapita

“Njama za kuvuruga uchaguzi mkuu” alisema Gavana

“Ndiyo mzee.”

“Nani hao wanaotaka kuvuruga uchaguzi mkuu? Aliuliza Gavana

“Kwa mujibu wa Regina uchaguzi huo unataka kuvurugwa na chama chake cha Ukombozi wa Afrika.Ni mpango unaofanywa kwa siri kubwa sana na alipogundua basi akatakiwa kuuawa” alijibu Mathew

“Ni namna gani wanataka kuuvuruga huo uchaguzi mkuu? Aliuliza Gavana

Mathew alimueleza Gavana kila kitu namna Regina alivyoweza kujua kuhusu uwepo wa mipango ya siri ya kuhujumu uchaguzi mkuu wa Rais na wabunge.

“Hiki ulichonieleza bwana Mathew kimenitetemesha sana.Sikufichi nimeogopa.Ni akina nani hawa wanataka kufanya jambo kama hili?” Aliuliza Gavana na kumtazama Mathew kwa wasi wasi.

“Kwa nini jambo hili msilifikishe katika vyombo vya

uchunguzi ili vilifanyie kazi kwa haraka? Aliuliza Gavana

“Tunazifanyia kwanza uchunguzi taarifa hizi za uwepo wa hujuma katika uchaguzi mkuu na tutakapothibitisha kweli zipo njama za kuvuuga uchaguzi basi tutafikisha taarifa hizo kwa vyombo husika.Kwa sasa tunaendelea na uchunguzi wetu kwa siri na ninakuomba nawe pia usimueleze mtu mwingine yeyote haya niliyokueleza.Tunataka kuwabaini wasaliti wa taifa hili.” Alisema Mathew

“Nimekuelewa Mathew hata hivyo inabidi muwe makini sana katika uchunguzi wenu kwani tuna kipindi kifupi sana hapa kabla ya uchaguzi mkuu hivyo juhudi za kuutafuta ukweli zinapaswa ziwe kubwa.” Alisema Gavana

“Tunalifahamu hilo mzee.Tunafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha ndani ya kipindi kifupi tunaupata ukweli” alisema Mathew

“Bwana Mathew,pamoja na kazi kubwa na ngumu ya kuutafuta mtandao huo

unaotaka kuhujumu uchaguzi mkuu,kuna jambo ninataka kukuomba unisaidie” alisema Gavana na kuvuta pumzi ndefu.

“Jambo gani mzee? Aliuliza Mathew

“Ninataka unisaidie kuupata ukweli kuhusu kupotea kwa mwanangu Kelvin.Mtu pekee ambaye nina uhakika kuna kitu anakifahamu kuhusu kupotea kwa Kelvin ni Regina ambaye kwa sasa unaye mikononi mwako.Ninakuomba umfanyie

uchunguzi wa kina yule mwanamke na vile vile uwe makini naye sana.Kuuawa kwa wapelelezi watatu wanaolichunguza suala la kupotea Kelvin ni ishara ya wazi kuwa tukio lile halikuwa la kawaida.Kuna siri kubwa nyuma yake na anayeifahamu siri hiyo ni Regina.Ninakuomba Mathew unisaidie kuupata ukweli kuhusu mwanangu.Nitakusaidia kwa chochote utakachokihitaji katika jukumu hilo.Mpaka hatua hii nimekwisha poteza

mamilioni ya fedha katika kuutafuta ukweli kuhusu kupotea mwanangu lakini mpaka sasa bado sijafanikiwa kuupata ukweli.Ninakuomba sana Mathew Mulumbi nisaidie katika hilo suala.Niko tayari kutumia kiasi chochote cha pesa katika kuusaka ukweli juu ya kupotea mwanangu.Nafahamu uchunguzi kama huu unahitaji fedha nyingi.Mimi nitabeba gharama zote za uchunguzi huu.” Alisema Gavana

“Ahsante sana Gavana.Ninakuahidi

nitakusaidia kuutafuta ukweli kuhusu mwanao.Kuhusu fedha usiwe na wasi wasi pale tutakapokuwa na uhitaji nitakujulisha mara moja.Ninachokuomba kuanzia sasa kuwa makini sana hasa na wale watu wanaokuzunguka.Inaonekana mambo yako yote unayoyafanya yanajulikana haraka sana ndiyo maana wapelelezi wote unaowaweka ili kuchunguza suala la kupotea mwanao wamekuwa wakiuawa haraka sana kabla hawajafika mbali katika

uchunguzi wao.Narudia tena kukuomba kwamba usimueleze mtu mwingine yeyote haya niliyokueleza.Ibaki siri yako.Baada ya kupiga hatua katika uchunguzi huu nitakuja kukupa mrejesho wapi tumefikia.Sitaki mawasiliano yetu yawe katika simu kwa sababu hatujui nani anafuatilia mawasiliano yako.”

“Unahisi wapo watu ambao wanafuatilia mawasiliano yangu ya simu ndiyo maana mipango yangu yote inagunduliwa mapema? Aliuliza Gavana

“Hilo linawezekana.Tutalifanyia uchunguzi pia.Hata hivyo kuwa makini sana na watu wako wa karibu” alisema Mathew.

“Ninakushukuru sana bwana Mathew kwanza kwa kufika hapa.Ninaamini safari hii nitaupata ukweli kuhusu suala la mwanangu kupotea.Ninaamini ni Mungu ndiye aliyekuleta kwangu ili unisaidie katika jambo hili.Naendelea kukusisitiza kuwa makini sana.Wewe na

wenzako ni muhimu sana kwa nchi hii.”alisema Gavana

Waliendelea na mazungumzo kidogo halafu Mathew akamuaga Gavana.

“Ahsante sana Gavana kwa muda wako.Nitayafanyia kazi yale yote uliyonieleza.Nitakupa mrejesho wa kile nitakachokipata” alisema Mathew huku akinyanyuka.Gavana alivuta droo ya kabati akatoa kadi yenye mawasiliano yake akamsindikiza Mathew hadi garini wakaagana

akaondoka.Gavana alitoa kitambaa akafuta jasho akabaki amesimama katika kibaraza hadi taa za gari la Mathew zilipofutika kabisa machoni pake.

“Ni nani yule kijana? Gavana alishtuliwa na sauti ya mke wake aliyekuwa amesimama mlangoni.

“Anaitwa Mathew Mulumbi.Ni mpelelezi ambaye amekuja kunipa taarifa kwamba Johnson ameuawa” alisema Gavana na kumshtua sana mke wake ambaye

alipeleka mkono wake mahali ulipo moyo.

“Johnson amefariki dunia? Aliuliza mke wa Gavana kwa hofu

“Ndiyo ameuawa.” Alisema Gavana na kumueleza mke wake kile alichoelezwa na Mathew.

“Ninaamini sasa suala la Kelvin ambalo limetutesa kwa muda mrefu linakwenda kupata majibu.Tumuombee sana yule kijana na wenzake kwani wanachokifanya ni kitu

cha hatari mno” alisema Gavana

****

Geti la nyumba walimoweka kambi akina Mathew lilifunguliwa,Mathew akaingiza gari ndani.Mara tu aliposhuka alikutana na Ruby.

“Ahsante umerudi.Nilikuwa najiuliza saa ngapi utarejea” alisema Ruby

“Kuna tatizo lolote lililokupa hofu? Aliuliza Mathew

“Sina amani kabisa kukaa ndani pamoja na yule Jombaa.Macho yake yanatisha” alijibu Ruby

“Usiogope.Hawezi akakufanya chochote.” alisema Mathew

“Mathew inakuaje unamuamini mtu kwa haraka namna hii? Alihoji Ruby

“Anaweza akawa na msaada kwetu siku Fulani.Watu kama hawa huwa wana msaada mkubwa sana” alisema Mathew

“Mathew tusiingie ndani naomba tukae hapa nje tuzungumze.Nataka unipe mrejesho wa ulichokipata huko ulikotoka.Umefanikiwa kuonana na Gavana? Aliuliza Ruby.Waliketi katika viti vilivyokuwa katika bustani ndogo.Mathew alimueleza Ruby kila kitu alichokizungumza na Gavana.

“Gavana yuko sahihi kabisa.Huyu Regina ni mwanamke hatari sana.Si kama tunavyomchukulia ! Alisema Ruby

“Kwa nini unasema hivyo Ruby? Mathew aliuliza

“Usiku huu baada ya kuwapatia chakula sikutaka kukaa ndani.Nilitoka nikazima taa ya nje nikaenda kujificha chini ya ule mti pale.Nilimuhofia Jombaa.Nikiwa pale chini ya mti nilisikia sauti ya muanguko wa kitu.Sekunde chache baadae niliona kama kivuli cha mtu akikimbia kuelekea upande wa nyuma ya nyumba.Niliambaa na ukuta nikiwa na ile bastola uliyoniachia nikihofu labda

tumevamiwa.Nilipochunguza vizuri nilimuona Regina akiwa katika yale mavazi uliyomnunulia akielekea katika mlango wa dharura kule nyuma ya nyumba.Alikuwa makini kutazama nyuma kama kuna mtu yeyote aliyemuona.Nilishangaa aliuvuta mlango ukafunguka akatoka nje.Inaonekana mchana tulipomuacha hapa alifanya uchunguzi wa nyumba hii na akaufungua ule mlango wa nyuma.Alipotoka nami nilitoka nikaendelea kumfuatilia kwa makini sana

bila yeye kufahamu kama anafuatiliwa.Alitembea haraka haraka huku akigeuka nyuma kuchunguza kama kuna mtu anamfuatilia.Alikwenda hadi katika kituo cha piki piki hapo mbele kidogo akaingia katika bajaji.Mimi nilichukua piki piki nikaanza kuifuatilia ile bajaji.Dakika kama kumi baadae alishuka katika ile bajaji akaingia katika taksi.Niliendelea kuifuatilia ile taksi aliyopanda Regina hadi karibu na baa Fulani silikumbuki jina lake.Ile taksi aliyopanda Regina ilisimama

na baada ya dakika kama saba ikatokea gari aina ya BMW yenye rangi nyeusi.Regina alishuka katika ile taksi akiangia katika ile BMW na kuondoka mahali pale.Niliendelea kufuatilia ile BMW nikiwa .” Ruby alinyamaza kidogo akameza mate kulainisha koo.

“Gari lile lilikwenda hadi katika nyumba moja nzuri sana.Jamaa mmoja aliyekuwa amevaa kaptura ya khaki na fulana ya iliyokatwa mikono alishuka garini akaenda kufungua geti kisha akarudi

garini na kuingiza gari ndani.Nilijibanza sehemu nikasubiri.Baada ya dakika ishirini gari lile lilitoka.Jamaa yule alishuka garini akaenda kufunga geti halafu akarudi garini na kuondoka.Gari lile lilirejea katika ile baa ambako Regina alishuka akachukua taksi.Niliamua kumfuata yule jamaa.Baada ya kuachana na Regina alikwenda Vega Night club.Sikumuacha niliendelea kumuandama.Niliingia ndani ya klabu ile ya usiku.Nilimshuhudia yule jamaa akiwa na wanawake

wawili makahaba.Kwa namna nilivyomuona hakuwa na mategemeo ya kuondoka mapema eneo lile hivyo niliamua kuondoka.Niliporejea hapa,Regina naye tayari alikuwa chumbani kwake.Mathew kwa asilimia mia moja ninakubaliana na Gavana mwanamke huyu ni hatari.Kwa namna alivyoweza kutoka humu ndani anaonekana wazi ni mtu mwenye mafunzo makubwa" alisema Ruby.

"Ruby ninakupongeza sana kwa kazi kubwa na ya

hatari uliyoifanya.” Alisema Mathew

“Ninakupongeza wewe kwa mafunzo yako kwani nimejifunza kwako namna ya kuweza kumfuatilia mtu” alisema Ruby huku akitoa kicheko kidogo.

“Huyo mtu ambaye Regina alikwenda kuonana naye usiku huu ni nani? Ni mume wake? Aliuliza Mathew.

“Sina hakika kama ni mume wake”

“Kama si mume wake ni nani? Anaonekana ni mtu muhimu sana kwa Regina hadi akaamua kuondoka usiku huu kumfuata bila kujali kama anatafutwa na jeshi la polisi.Lazima tumchunguze sana Regina.Kwa kuanzia tunaanza na huyu mtu aliyekwenda kuonana naye usiku huu.Tukimpata huyo nina uhakika tutapata mambo muhimu ya kumuhusu Regina na hasa sababu ya kwenda kuonana naye usiku huu.Hakuna kitu kingine umekipata? Aliuliza Mathew.

“Hapana sijapata chochote” alijibu Ruby

“Hakuna tatizo,usiku huu tutamfuata yule jamaa nyumbani kwake.Nina uhakika lazima atakuwa ni mtu muhimu kwa Regina.Atatusaidia sana” alisema Mathew na kuingia ndani ili kujiandaa kabla ya kwenda kumfuatilia mtu aliyekutana na Regina usiku ule.

****

Mlango wa chumba alimofungwa Gosu Gosu ulifunguliwa wakaingia watu wanne.Hawakumsemesha chochote walifungua mikanda ya kitanda iliyokuwa imemfunga barabara.Bado alihisi maumivu kutokana na dawa ile ya maumivu aliyochomwa wakati akiteswa.Baada ya kumfungua wale jamaa walimfunga pingu wakamfunika mfuko kichwani wakamtoa mje.Aliingizwa katika gari na safari

ikaanza.Hakufahamu mahali alikokuwa anapelekwa.

Mwendo wa dakika Thelathini gari lile lilisimama,mlango ukafunguliwa Gosu Gosu akashushwa garini akaongozwa kuelekea ndani ya nyumba.Aliingizwa ndani ya chumba akafunguliwa zile pingu za mikono halafu akaachwa mle chumbani.

“Nimemuingiza Mathew Mulumbi katika matatizo makubwa sana.Hawa jamaa ni watu wabaya lazima watafanya

kila lililo ndani ya uwezo wao kuhakikisha wanampata.Wana hofu ataharibu mipango yao yote.Siko tayari kuwasaidia kumpata Mathew hata kama itanigharimu uhai wangu.Jambo lingine linalokula akili yangu ni juu ya mpenzi wangu Ambola.Ni kweli atakuwa ameuawa? Kwa nini yule mwanamke akafanya ukatili mkubwa namna ile kwa mwanae? Je Ambola anafahamu kama ninashikiliwa mateka na mama yake? Natamani sana kumuokoa lakini ninashindwa

nitamsaidiaje kwani nimefungwa halafu sifahamu mahali alipo.”Gosu Gosu alitolewa mawazoni baada ya mlango kufunguliwa akaingia Bernadetha mama yake Ambola.Gosu Gosu alipatwa na hasira za ghafla akasimama.

“Relax darling” alisema Bernadetha ambaye hakuonesha hata chembe ya wasiwasi.

“Unafahamu lakini kama ninaweza kukuua kwa mikono yangu sasa hivi? Aliuliza Gosu Gosu kwa ukali.

“Ninafahamu lakini huwezi kufanya hivyo.Please sit down” alisema Bernadetha.Bado Gosu Gosu aliendele kumtazama kwa hasira.

“Haya ndiyo malipo kwa yote niliyokufanyia? Aliuliza Gosu Gosu

“Gosu Gosu nimekuja kwa mara nyingine tena kuzungumza nawe.Hatima yako itategemea sana utulivu wako na namna utakavyokubaliana nami” alisema Bernadetha lakini

kabla hajaendelea Gosu Gosu alimkatisha.

“Hatuna cha kuzungumza.Mimi nawe tumemalizana.Ulinipa kazi ya kufanya nimeifanya lakini malipo yake ni haya ya kunifunga na kunitesa namna hii.Ninataka unitazame usoni vizuri wakati ninakutamkia haya maneno” alisema Gosu Gosu akiendelea kumtazama Bernadetha kwa hasira

“Niue wakati bado una nafasi.Ukichelewa sasa na kuniacha nikapata nafasi

nitakumaliza wewe na mtandao wako wote ! alisema Gosu Gosu.Bernadetha alijitahidi kutabasamu licha ya maneno yale kumpa hofu kubwa.

“Gosu Gosu vitisho haviwezi kukusaidia kwa lolote.Mimi sina lengo baya kwako.Ninataka nikusaidie.Ninakutengenezea maisha mazuri.Sikiliza Gosu Gosu.Haya yote yasingetokea kama usingeharibu kazi kwa kumuhusisha Mathew Mulumbi.Ulikosea sana ulipomuhusisha Mathew

Mulumbi katika kazi niliyokupa.Hukupaswa kufanya vile.Kwa sababu yako yule mwanamke hadi sasa hatufahamu mahali alipo .Labda tu nikueleze kwamba yule mwanamke ni hatari kwa usalama wa taifa.Hatakiwi hadi sasa awe anavuta hewa hii safi.Kitendo cha wewe kushindwa kumuua na kumshirikisha Mathew Mulumbi kinazidi kuliweka taifa hili katika hatari kubwa.Tunachohitaji kwa sasa tusaidie kumpata Mathew Mulumbi ili tuweze kumpata

yule mwanamke.Tukimpata huyo mtu basi hatutakuwa na shida nawe tena tutakuacha ukaendelee na maisha yako.Jambo zuri ni kwamba Mathew atakapoondolewa basi kila kitu alichonacho kitabaki mali yako.Wewe ndiye mshirika wake mkubwa na amekuamini sana.Unaonaje kama mali zote zitakuwa zako pale utakapotusaidia kumpata Mathew Mulumbi? Aliuliza Bernadetha.Gosu Gosu alimtazama kwa dharau halafu akatema mate chini.

“Stupid ! alisema Gosu Gosu

“Gosu Gosu litumie vyema hili dirisha.Utaijutia nafasi hii uliyoipata baadae” alisema Bernadetha

“Wewe ndiye unayepaswa kulitumia dirisha hili kuniua.Utajuta kuitumia vibaya nafasi hii” alisema Gosu Gosu.Bernadetha alimtazama kwa makini sana halafu akainuka akatoka ndani ya kile chumba.

“Nimemwambia ukweli hawatapata chochote kutoka

kwangu na kama ikiwezekana ni vyema kama wataitumia nafasi hii wakanimaliza lakini wakishindwa na kuniacha nikapata upenyo hata mdogo,wamekwisha” aliwaza Gosu Gosu baada ya Bernadetha kutoka mle chumbani.

Zilipita dakika tano mlango ukafunguliwa wakaingia watu wanne mmoja wao akiwa na bastola.Alimuelekezea Gosu Gosu akamtaka kuinua mikono juu.Gosu Gosu alitii akainua mikono juu mmoja wa wale

jamaa akazunguka akamshika mkono akamfunga pingu halafu wakamvalisha mfuko kichwani wakamtoa ndani ya kile chumba.Aliingizwa tena katika gari milango ikafungwa gari likaondoka.Baada ya mwendo wa dakika kadhaa gari lile lilisimama Gosu Gosu akashushwa akaingizwa ndani.Alikalishwa katika sofa nzuri pingu zikafunguliwa halafu ule mfuko kichwani ukatolewa.Gosu Gosu hakuamini kile alichokiona mbele yake.

“This is not true ! alisema Gosu Gosu.

****

Ruby alikumbuka vyema mahali ambako Regina alikwenda usiku ule hivyo alimuongoza Mathew hadi mahali hapo.Mathew aliendesha gari taratibu huku wakiichunguza kwa makini sana ile nyumba.Katika geti bado kulikuwa na kufuli kubwa.

“Kuna kufuli getini.Inaonesha yule jamaa bado hajarudi nyumbani”

alisema Ruby.Waliegesha gari mita kadhaa kutoka ile nyumba.Walishuka na kutembea taratibu kuelekea katika geti la ile nyumba.Kulikuwa na watu wachache waliokuwa wanapita lakini Mathew hakuwajali aliliendea kufuli akatoa vyuma viwili vidogo vyenye ncha kali akaanza kulichokonoa kufuli.Baada ya sekunde chache kufuli lilifunguka.Alifungua geti akaingia ndani.Ruby ambaye alibaki nje alilifunga lile kufuli

halafu akarejea katika gari lao kumsubiri Mathew.

Nyumba ilikuwa kimya kabisa.Hakukuwa na dalili yoyote ya kuwepo mtu ndani.Taa mbili zilizokuwa mbele ya ile nyumba zilikuwa zinawaka.Taratibu na kwa tahadhari Mathew alipanda katika kibaraza akausogelea mlango akatumia vile vifaa vyake akafungua kitasa cha mlango akaingia ndani.Kwa kutumia kurunzi ndogo alimulika pale sebuleni.Kulikuwa na sofa za gharama kubwa na runinga

kubwa iliyotundikwa ukutani.Kulikuwa pia na kabati ambalo ndani yake kulikuwa na vitabu kadhaa lakini sehemu kubwa ilikuwa tupu.Alilifungua kabati lile akamulika hakupata kitu akatoka akaingia katika chumba cha chakula akatokea jikoni halafu akafunua pazia akafuata korido.Kulikuwa na milango minne kuashiria nyumba ile ilikuwa na vyumba vitatu vya kulala.Alifungua mlango uliokuwa karibu na jiko kilikuwa ni choo.Alifunga akapiga hatua kadhaa akaenda

katika mlango mwingine.Ulikuwa umefungwa kwa funguo.Akachokonoa kitasa akaufungua.Kilikuwa ni chumba kikubwa cha kulala.

“Hiki lazima kitakuwa ni chumba chake cha kulala.” Aliwaza Mathew

Ndani ya kile chumba kulikuwa na kitanda kikubwa,sofa moja rangi nyeusi na runinga kubwa ukutani.Kulikuwa pia na milango mingine mitatu ndani ya kile chumba.Mathew aliufungua mlango wa kwanza

kilikuwa ni choo.Alifunga akaufungua mlango wa pili kilikuwa ni chumba maalum kwa ajili ya mavazi.Kulikuwa na makabati makubwa mawili yaliyojaa nguo zilizopangwa katika mpangilio nadhifu kabisa.Vile vile kulikuwa na kabati lenye kioo kikubwa.Alivuta droo za kabati lile hakupata kitu zaidi ya chupa zilizomalizika uturi.Alitoka ndani ya kile chumba akaufungua mlango wa tatu ulikuwa umefungwa kwa funguo.Hakupoteza muda

akatumia vile vifaa vyake akaufungua ule mlango.

“Hakuna kufuli au kitasa katika dunia hii ambacho kitanishinda kufungua.” Aliwaza na kuwasha kurunzi yake ile ndogo lakini yenye mwangaza mkali.Kitu cha kwanza alichokiona ni meza iliyokuwa na kompyuta mpakato.Aliisogelea meza ile akakutana na makaratasi mengi yaliyozagaa pale mezani.Aliyachunguza halafu akafungua moja ya droo za ile meza.Alikutana na mafungu

manne yaliyofungwa yenye hati za kusafiria.

“Hati hizi ni kwa ajili gani? alijiuliza Mathew akiendelea kuzikagua.Mara mwangaza mwekundu uliwaka mara tatu katika saa aliyokuwa ameivaa.Hii ilikuwa ni ishara kutoka kwa Ruby kuwa yule jamaa anarejea.Haraka haraka alizirudisha zile hati katika kabati akatoka akaingia katika chumba cha mavazi akajificha.

Baada ya dakika chache mlango ulifunguliwa akasikia sauti ya mwanaume mmoja na

wanawake wawili wakiingia ndani ya kile chumba.

“Karibuni ndani” ilisema sauti ya mwanaume akionekana alikuwa amelewa.

“Inno nyumba yote hii kwa nini unaishi mwenyewe? Aliuliza mwanamke kwa sauti nyororo

“Acha kufuatilia maisha yangu wewe” alisema yule jamaa kwa sauti ya kilevi.

Akiwa ndani ya kile chumba alisikia viatu vikirushwa sakafuni.

“Inaonekana wamelewa sana hawa watu” aliwaza Mathew.

“Kuna yeyote anataka kuendelea kunywa pombe? Nina pombe nyingi humu ndani” aliuliza yule jamaa.

“Tukilewa sana tutashindwa kukuburudisha.” Alisema mmoja wa wale wanawake

“Kweli Inno.Tustarehe kwanza halafu baadae tutakunywa pombe.Leo hakuna kulala”.

“Okay.Welcome ladies” alisema yule jamaa.Mathew alichungulia kupitia kitobo cha funguo akamuona yule jamaa akiwa amelala kitandani huku wale wanawake wawili waliovalia nusu utupu wakianza kumvua nguo.Baada ya kumvua mavazi yule jamaa,wale wanawake nao walivua mavazi wakabaki watupu.Mmoja alikuwa upande wa kulia na mwingine kushoto.

“Hii kitaalamu inaitwa *threesome*.Ni bahati mbaya wataikatisha starehe yao”

aliwaza Mathew na taratibu akaufungua mlango akatoka.Watu wale kitandani ni kama vile walikuwa katika dunia nyingine kabisa.Hawakuwa na habari kama kuna mtu alikuwa amesimama akiwatazama.

“Hey ! alisema Mathew lakini wale jamaa ni kama vile hawakusikia kitu.Aliisogelea swichi ya kuwashia taa akaizima na kuwasha.Kitendo kile kiliwashitua watu wale waliozama katika starehe yao.

“Hey ! alisema tena Mathew na yule jamaa ambaye alikuwa wa kwanza kumuona Mathew alimsukuma mwanamke mmoja pembeni akanyanyuka kwa haraka.

“Kaa hapo hapo ulipo.! Aliamuru Mathew

“Mam…..” mwanamke mmoja alitaka kupiga kelele baada ya kumuona Mathew akiwa na bastola.Ulikuwa ni kama muujiza kwao.Waliinua mikono yao juu.

“Ninyi wanawake nyanyukeni haraka” alisema

Mathew na kwa haraka wanawake wale wawili walinyanyuka.Walikuwa watupu.Miili iliwatetemeka kwa hofu.Kiumbe waliyekuwa wanatazamana naye hakuonekana kuwa na hata chembe ya huruma.

“Ingieni chooni ! aliamuru Mathew.Haraka haraka waliingia chooni.Mathew akamuamuru yule jamaa kuvaa nguo.

“Kaka naomba sana usiniue tafadhali.Niko chini ya

miguu yako” alisema yule jamaa

“Vaa nguo zako haraka sana ! alifoka Mathew.

“Brother nakuomba nik…..” alisema yule jamaa akiwa amepiga magoti baada ya kuvaa bukta yake.

“Simama ! aliamuru Mathew,akakata waya akamtaka yule jamaa aingie chooni akawafunga wale wanawake barabara.Kama haitoshi alichana fulana akamtaka ajaze matambara

midomoni mwao ili wasiweze kupiga kelele.”

“Hiyo ni stahili yenu ili mkitoka hapa mkajifunze kufanya kazi za halali kuliko kuuza miili yenu.! Alifoka Mathew na kutoka mle chooni akamuamuru yule jamaa kuelekea katika kile chumba ilimo kompyuta.

“Washa taa” aliamuru Mathew yule jamaa kwa haraka akawasha taa,Mathew akamtaka aketi kitini

“Broth….” Alitaka kusema kitu yule jamaa,Mathew akamzuia.

“Shut up ! alisema Mathew akiendelea kumtazama yule jamaa aliyekuwa akitetemeka kwa hofu

“Jina lako nani? Aliuliza Mathew

“Naitwa Innocent Sungura” alijibu yule jamaa

“Unafanya kazi gani Innocent?

“Sina kazi maalum.”alijbu yule jamaa.

“Fungua droo ya kabati haraka” alisema Mathew.Innocent alifanya kama alivyoamriwa,alifungua droo ya kabati.

“Hizo hati za kusafiria zinafanya nini humu? Aliuliza Mathew.Innocent hakujibu kitu.Midomo ilimtetemeka.

“Nakuuliza kwa mara ya mwisho hizi hati za kusafiria zinafanya nini humu ndani? Aliuliza Mathew kwa ukali.

“Brother nitakueleza ukweli.Hizi hati ni bandia ambazo huwatengenezea watu

mbali mbali wanaotafuta” alijibu Innocent huku akitetemeka.

“Unafahamu kama hilo ni kosa la jinai? Aliuliza Mathew

“Ninafahamu brother naomba unisamehe.”

“Mimi sijakuhukumu,nitakufikisha sehemu husika ambako utapata adhabu unayostahili kwa kosa hili la kutengeneza hati bandia za kusafiria.”

“Naomba unisamehe brother.” Innocent aliendelea kuomba.

“Innocent kuna jambo ambalo nataka tuzungumze na kama ukinieleza ukweli mtupu basi nitakuacha salama lakini kama ukinidanganya sasa hivi polisi watafika hapa nyumbani kwako kukuchukua” alisema Mathew

“Nitakueleza ukweli brother” alisema Innocent.

“Usiku huu kabla hujakwenda klabu ambako umewatoa hawa makahaba

uliokuja nao,ulikwenda sehemu fulani ukamchukua mwanamke mmoja ukamleta hapa na baada ya dakika kadhaa ukaondoka naye ukamrejesha mahali ulipomtoa.Unakubali? aliuliza Mathew.Sura yake ilizidi kumuogopesha Innocent.Alifikiri kidogo halafu akasema

“Ni kweli brother.”alijibu Innocent

“Ninataka uniambie ukweli kuhusu yule

mwanamke ni nani? Aliuliza Mathew

“Anaitwa Regina.Ni naibu katibu mkuu wa chama cha ukombozi wa Afrika.” Alijibu Innocent

“Unaweza ukaniambia alikuja kutafuta nini hapa kwako usiku huu? Aliuliza Mathew.

“Alikuja kuomba msaada” alijibu Innocent.

“Msaada gani aliokuja kukuomba? Mathew

aliuliza.Innocent aliogopa kujibu akabaki kimya.

“Innocent ninataka nikikuuliza kitu unajibu haraka.Ukiniudhi utajikuta sehemu mbaya sana.Nataka kufahamu msaada gani ambao Regina alikuja kukuomba? Aliuliza Mathew

“Alikuja kuomba…” alisema Innocent halafu akasita.

“Alikuja kuomba nini? Mathew aliuliza

“Regina alikuja kuomba nimsaidie kupata hati ya kusafiria” alijibu Innocent

“Alikwambia anahitaji hati hiyo kwa ajili gani? aliuliza Mathew

“Alinieleza kwamba anatafutwa na jeshi la polisi kwa tuhuma za mauaji ambayo hakuyafanya.Aliomba nimsaidie kutengeneza kwa haraka sana hati ya kusafiria ili aweze kuondoka nchini” alisema Innocent

“Alisema anataka kuelekea wapi? Aliuliza Mathew

“Kisiwa cha Zales”

“Alikwambia kwa nini anataka kwenda Zales? Aliuliza Mathew

“Anaamini kule ndiko atakuwa salama.” Alijibu Innocent

“Umempa jibu gani?

“Nimeahidi kumsaidia.”

“Atakulipa kiasi gani kwa kazi hiyo? Aliuliza Mathew

“Nilimwambia anipe shilingi milioni mbili akaniambia atanipa milioni

tano nimfanyie haraka haraka” alijibu Innocent

“Lini atakupatia hizo fedha alizokuahidi? Aliuliza Mathew

“Ameahidi atanitumia atakapofika Zales.Kwa hapa Tanzania hawezi kuchukua fedha katika akaunti yake akihofia kufuatiliwa” alijibu Innocent

“Umefahamiana lini na Regina? Mathew aliuliza

“Tumefahamiana tangu tukiwa chuo kikuu”

“Umewahi kufika nyumbani kwake? Aliuliza Mathew

“Ndiyo nimefika” alijibu Innocent.

“Unamfahamu mume wa Regina? Aliuliza Mathew.Innocent alishindwa kujibu.

“Innocent nakuuliza unamfahamu mume wa Regina? Aliuliza Mathew.

“Regina hana mume.Aliyekuwa mpenzi wake alipotea katika mazingira tata

na hadi leo hii hajaolewa tena.Anaishi peke yake” alijibu Innocent.

“Ahsante kwa kutoa ushirikiano.Haya niliyokuuliza yabaki siri yako usimwambie mtu yeyote.Endelea na shughuli zako kama kawaia kwani hata mimi ninaweza kuhitaji msaada wako siku Fulani.Nataka uendelee kumtengenezea Regina hati ya kusafiria kama alivyokuomba.Narudia tena usimweleze chochote kuhusiana na haya

niliyokuuliza.Umenielewa? aliuliza Mathew

“Nimekuelewa brother.”alijibu Innocent.

“Nipe namba yako ya simu” alisema Mathew na haaka haraka Innocent akamuandikia namba yake ya simu.

“Utawasiliana vipi na Regina kumjulisha kuwa kazi yake imekamilika? Aliuliza Mathew

“Kwa sasa hana simu ila tumekubaliana baada ya siku

mbili atakuja hapa kufuatilia kama kazi yake imemalizika” alijibu Innocent

“Leo mliwasilianaje? Mathew aliuliza

“Alitumia simu ya dereva taksi kunipigia ndipo nikamfuata mahali aliponielekeza”alijibu Innocent

“Ahsante kwa ushirikiano.Nitakuwa mgongoni kwako nikikufuatilia.Kama utamueleza Regina au mtu yeyote haya niliyokuuliza nitafahamu na utakuwa katika

wakati mgumu sana.” Alisema Mathew halafu akamtaka watoke.Bado Innocent alikuwa anatetemeka.Alimfungulia Mathew geti akatoka.

“Tutaonana tena muda wowote” alisema Mathew akaifutika bastola yake kiunoni akaondoka.Innocent alifunga geti haraka haraka akarudi ndani akikimbia.Hakuamini kama alikuwa salama.Kitu cha kwanza alichokifanya ni kukimbilia chooni kuwafungua wale makahaba wake wawili akawataka wavae nguo zao haraka waondoke mahali pale.

Mathew alirejea katika gari lao ambako alimkuta Ruby akimsubiri.Aliwasha gari wakaondoka.

Wakiwa njiani kurejea nyumbani kwao,Mathew alimueleza Ruby kila kitu alichokipata kutoka kwa Innocent.

“Imekuwa vyema tumeifahamu mipango yake kabla haijafanikiwa.Zales anakotaka kukimbilia Regina ni wapi?” aliuliza Ruby

“Zales ni kisiwa tajiri sana.kina utajiri mkubwa wa

mafuta na gesi.Zales inaitwa pepo ya dunia kutokana na uwingi wa starehe zinazopatikana katika kisiwa hicho.Kingine kikubwa kuhusu kisiwa hicho ni mahali ambako mafisadi,wauzaji dawa za kulevya na wafanya biashara zote haramu huficha hedha zao.Ukisikia mtu ana akaunti ya fedha Zales basi amini kwa asilimia kubwa fedha hiyo si halali.Ni sehemu ambayo wengi huitumia kufichia fedha.Regina amemuahidi Innocent kwamba atamtumia fedha yake akifika Zales

ambako ana akaunti hii inatoa picha kuwa kuna fedha amezihifadhi huko.Tuendelee kumchunguza tutafahamu mengi” alisema Mathew.

Walirejea katika makazi yao,Ruby akaelekea ofisini Mathew akaenda katika chumba cha Jombaa kujua maendeleo yake.Baada ya hapo alikwenda katika chumba cha Regina akagonga mlango lakini hakujibiwa.Aligonga mara ya pili lakini hakujibiwa akakinyonga kitasa akaufungua mlango.Regina alikuwa amepitiwa na

usingizi.Mathew alimsogelea akamuamsha.

“Mathew” alisema Regina

“Amka ninahitaji kuzungumza nawe” alisema Mathew na kutoka.Regina aliamka akavaa na kutoka nje ambako alimkuta Mathew akimsubiri wakaelekea sebuleni.

“Regina tukiwa Arusha ulihitaji simu ili uwasiliane na mume wako kumfahamisha kuwa uko salama.Tunataka kukupatia simu uzungumze

naye umjulishe uko sehemu salama” alisema Mathew

“Nawashukuru sana kwa msaada huo.Mume wangu atakuwa katika wakati mgumu sana hivi sasa baada ya taarifa zangu kusambaa kuwa ninasakwa na jeshi la polisi kwa mauaji” alisema Regina.

Mathew aliinuka akaenda katika chumba cha ofisi alimo Ruby.

“Kila kitu tayari? Aliuliza

“Kila kitu tayari” alijibu Ruby na kumpatia simu Mathew akampelekea Regina.

“Kuwa huru kuzungumza naye lakini usimueleze mahali ulipo,au uko na akina nani.Umenielewa? aliuliza Mathew

“Nimekuelewa” alijibu Regina.

“Good.Kuwa huru” alisema Mathew na kutoka pale sebuleni akamuacha Regina akiandika namba ya simu ya mume wake.Mathew alirejea ofisini aliko Ruby na

wote walivaa spika za masikioni.Katika kompyuta ya Ruby kulikuwa na program maalum iliyounganishwa na ile simu aliyokuwa anaitumia Regina.

“Mbona anapiga namba ile ya simu aliyokupa Innocent? Aliuliza Ruby

“Shhhhh ! Mathew alimfanyia ishara Ruby asubiri

Simu iliita na kupokelewa.

“Hallow” ilisema sauti ya Regina

“Hallow.Nani mwenzangu? Aliuliza jamaa upande wa pili

“Umesahau sauti hii ? Regina hapa”

“Ouh kumbe ni wewe.Unasemaje Regina? Umefika salama?

“Niko salama kabisa.”

“Unasemaje Regina?

“Nimekupigia kukujulisha kuwa nitakuwa nikitumia simu hii mara moja moja kuwasiliana nawe.” Alisema Regina.

“Sawa Regina.Kesho nitaanza kushughulikia ile kazi yako.” Alisema Innocent

“Nashukuru sana Innocent kwa msaada wako mkubwa” alisema Regina

“Regina” aliita Innocent na kusita

“Unasemaje Innocent? Aliuliza Regina

“Kuna jambo limetokea usiku huu” alisema Innocent.Ruby na Mathew walitazamana.

“Huyu mshenzi anamueleza Regina kila kitu.Kata simu haraka sana” alisema Mathew huku akitoka kwa kasi mle chumbani.

“Jambo gani limetokea Innocent? Aliuliza Regina

“Kuna watu wanakufuatilia kila unachokifanya” alisema Innocent

Kwa kutumia program ile Ruby alikata simu haraka sana.

“Nani wanaonifuatilia Innocent? Aliuliza Regna lakini hakupta mrejesho

“Hallow ! Hallow ! aliita Raegina halafu akaitazama simu akagundua tayari imekatwa.

“Naomba hiyo simu” ilisikika sauti ya Mathew Mulumbi aliyeingia kwa kasi pale sebuleni.Baada ya Regina kumkabdihi simu,Mathew alimtaka aketi sofani.

“Tayari umewasiliana na mume wako? Aliuliza Mathew

“Ndiyo” alijibu Regina lakini akionekana kuwa na wasiwasi mwingi.

“Innocent ndiye mume wako? Aliuliza Mathew

“Innocent? Aliuliza Regina kwa mshangao.

“Ni nani huyo Innocent? Aliuliza tena

“Nakuuliza ndiye mume wako? Mathew naye aliuliza

“Simfahamu huyo mtu.Mume wangu haitwi Innocent.” Alijibu Regina.

“Anaitwa nani mume wako?

“Anaitwa Chris”

“Uliyekuwa unazungumza naye simuni ndiye mumeo Chris? Aliuliza Mathew

“Ndiyo.Ni mume wangu”

“Tayari umemjulisha kuwa uko salama? Aliuliza Mathew

“Ndiyo nimemwambia niko salama asihofu” alijibu Regina.

“Good.”alijibu Mathew na kubonyeza kitufe katika saa

yake na baada ya sekunde chache akatokea Ruby.

“Regina ninataka utuambie ukweli.Je ni kweli ulikuwa unazungumza na mume wako? Aliuliza Mathew

“Ndiyo nilikuwa nazungumza na mume wangu.Kuna nini kwani? Hamniamini ? aliuliza Regina kwa ukali kidogo.Mathew alimpa Ruby ishara Fulani akacheza mazungumzo ya Regina na Innocent.Jicho la Regina lilizunguka kwa haraka kama Tai akiangalia kama

angeweza kupata upenyo wa kuchomoka mahali pale.Alitamani angegeuka upepo apotee.

“Regina huna cha kujitetea tena.Uongo wako umebainika na sasa naomba utueleze ukweli lakini kabla ya kusema chochote nataka nikwambie kwamba usiku huu nimetoka kuonana na Innocent” alisema Mathew.Sura ya Regina ilibadilika.Alianza kutetemeka.

“Nimeonana na Innocent.Nimezungumza naye.Amenieleza kila kitu

kuhusu mipango yako.” Alisema Mathew na kumueleza Regina kuhusu mipango aliyokuwa anaipanga.Regina midomo ilimtetemeka.

“Tumefahamu kuwa huna mume bali lengo lako lilikuwa ni kuwasiliana na Innocent ili akutengenezee hati ya kusafiria uondoke nchini.Regina sisi lengo letu si baya kwako.Tunataka kukusaidia.Ukitueleza ukweli tuko tayari hata kukusaidia kwenda huko Zales unakotaka kwenda.Ulitueleza kuna mipango ya kuvuruga uchaguzi

mkuu,tunaamini bado hujatueleza ukweli wote kuhusu jambo hili.Tueleze ukweli tafadhali na sisi tutakusaidia” alisema Mathew.

Regina alifuta machozi akainama chini.

“Regina narudia tena kukuhakikishia kwamba sisi hatutaki kuingilia maisha yako binafsi.Tunachohitaji sisi ni kufahamu ukweli halisi kwa nini unataka kuuawa nani wanataka kukuua na mipango ipi inapangwa kuvuruga uchaguzi mkuu.” Alisema

Mathew.Zilipita sekunde kadhaa za tafakari kisha Regina akainua kichwa akasema

“Nitawaeleza ukweli” Alinyamaza kidogo.

“Good.Usifiche kitu tafadhali” alisema Mathew.Walimpa Regina muda kidogo akatafakari kisha akasema

“Kufuatia mfululizo wa matukio ya vurugu na uvunjifu wa amani yaliyosababishwa na vyama vya upinzani,Rais aliiagiza idara ya siri ya

usalama wan chi inaitwa SANA kuvifanyia uchunguzi vyama vyote vya siasa nchini.Katika uchunguzi wao SNSA walibaini kwamba baadhi ya vyama hasa vile vikubwa ambavyo vilikuwa chanzo za vurugu nyingi vilikuwa na wafadhili nje ya nchi ambao waliwapatia misaada ya kifedha na vifaa kwa ajili ya kuendesha vyama vyao.Ilibainika kuwa baaadhi ya vyama hivyo vilipewa maelekezo ya kuchoche vurugu nchini kwa lengo la kuondoa amani na utulivu.Baada ya

kuipokea taarifa hiyo,Rais wa wakati huo alitoa maelekezo ya kuanzishwa kwa chama kikubwa cha upinzani ambacho kitakuwa na nguvu kubwa kuliko vyama vingine vya upinzani.Lengo la kuanzishwa kwa chama hicho ni kuvimaliza kabisa vyama vingine vya upinzani nchini.SNSA walipewa jukumu hilo.Hapo ndipo kilipoanzishwa chama cha ukombozi.” Regina alinyamaza akawatazma akina Mathew

“Mara tu chama hicho kilipoanzishwa kilianza kupata

umaarufu baada ya vigogo kuanza kuhama kutoka chama tawala na kuhamia katika chama hicho.Hama hama hiyo ya vigogo kutoka chama tawala iliwavutia pia hata viongozi kutoka katika vyama vingine vya upinzani ambao walivihama vyama vyao wakahamia chama kipya cha ukombozi.Taratibu lengo la kuanzishwa chama kile lilianza kutimia baada ya chama cha ukombozi kugeuka kuwa chama kikuu cha upinzani nchini.Vyama vingine vilianza kuzorota na kupoteza

wanachama wengi.” Alisema Regina akanyamaza tena.

“Endelea tunakusikiliza” alisema Mathew

“Chama cha ukombozi kilibaki chama pekee kikubwa cha upinzani nchini.Kilikuwa na wabunge zaidi ya mia moja katika bunge la jamhuri ya muungano wa Tanzania.Tofauti na vyama vingine vya upinzani,wabunge wa chama hicho hawakuipinga serikali bali waliiunga mkono na kuikosoa pale ilipobidi.Rais Malaki Augustine Mnambara

alipokaribia kumaliza kipindi chake cha pili cha uongozi alianzisha vugu vugu la mabadiliko ya katiba ili atawale vipindi vitatu badala ya viwili.Kwa bahati mbaya chama chake kiligoma kumuunga mkono Rais Malaki katika suala hilo.Kitendo hicho kilimuudhi sana Rais huyo na alipomaliza muda wake alianza harakati za siri na kukibomoa chama cha ukombozi na kikaundwa chama kipya cha Ukombozi wa Afrika ambacho kilishika hatamu ya kuwa chama kikuu cha upinzani

nchini.” Alinyamaza akameza mate halafu akaendelea.

“Serikali waligundua kwamba Rais mstaafu Malaki alikuwa anakisaidia chama cha Ukombozi wa Afrika kwa siri.Hapo ndipo kashfa mbali mbali za ufisadi na matumizi mabaya ya madaraka zilianza kuibuliwa zikimuhusisha Rais aliyemaliza muda wake Malaki Mnambara.Kwa mara ya kwanza Rais aliyemaliza muda wake alishtakiwa mahakamani kwa ufisadi na matumizi mabaya ya madaraka.Wakati kesi ikiendelea,Rais mstaafu

Malaki alianza kuumwa hivyo kupelekwa nje ya nchi kwa matibabu zaidi.Picha mbali mbali za Rais huyo akiwa hospitali akitibiwa zilianza kuonekana.Baada ya mwezi mmoja ilitangazwa kwamba mzee Malaki alifariki dunia.” Regina alinyamaza tena kwa muda.

“Kifo cha Rais Malaki kilizua utata mkubwa.Utata uliibuka pale ambapo familia ya marehemu waliamua kutourudisha mwili wake nyumbani wakauzika nje ya nchi.Japo taarifa ya kitabibu

na mamlaka za nchi alikofia zilithibitisha kuwa Rais mstaafu Malaki alifariki dunia na kuzikwa huko,zipo tetesi ambazo hadi leo hazijathibitishwa kuwa Rais huyo mstaafu yuko hai bado.Hakuna aliyewahi kuthibitisha hilo.Kwa maelezo hayo niliyowapa mtaona kuwa chama hiki cha Ukombozi wa Afrika ni chama chenye siri nyingi.Niliwaeleza kuhusu mtu anaitwa mfadhili ambaye hadi leo hii hafahamiki ni nani.Jambo lingine ni hili la

kuvuruga uchaguzi mkuu hasa wa Rais” alisema Regina

“Tuhamie hapo katika kuvuruga uchaguzi mkuu wa Rais.Tunahiaji utueleze ukweli nini hasa wamepanga kukifanya kuvuruga uchaguzi? Aliuliza Mathew

“Mipango iliyopo ni kwamba mgombea wa chama cha Ukombozi wa Afrika kwa namna yoyote lazima ashinde urais.Kama hilo litashindikana basi uchaguzi utavurugwa.Namna gani watafanya mgombea wao

ashinde au uchaguzi utavurugwa vipi hiyo ni siri kubwa ya viongozi wakuu wa chama ambayo Amani alikuwa anaitafuta lakini wamemuua kabla hajanieleza chochote.” alijibu Regina

“Nini hasa sababu ya wewe kutaka kuhama chama? Ruby aliuliza.

“Bado umri wangu mdogo na bado nina malengo makubwa kisiasa hivyo kwa mwelekeo wa chama changu ulivyo niliona namna malengo yangu kisiasa yanavyoyeyuka

kama barafu.Nyota yangu tayari imeanza kuwaka lakini kwa mwelekeo huu wa chama inakwenda kuzimika ndiyo maana nilianza mazungumzo na viongozi wa chama kilicho madarakani ili nihamie katika chama chao kabla ya uchaguzi mkuu" alijibu Regina

"Inaonesha hawa jamaa walikuwa wanakufuatilia kila ukifanyacho.Walifuatilia mawasiliano yako wakagundua ulikuwa unawasiliana na Amani,walifahamu pia mipango yako ya kuhama chama ndiyo maana

wakapanga kukuua.Unadhani kwa nini walikuwa wanakufuatilia? Aliuliza Mathew

“Ipo sababu ya pili ambayo inanifanya nitake kuhama chama.Niliwaeleza kuwa nilikuwa na mahusiano na Kelvin mtoto wa Gavana.Kuna wakati mimi naye tuliwahi kutengana baada ya kugundua alikuwa na mahusiano na mwanamke mwingine.Tulitengana kwa kipindi cha mwaka mmoja halafu tukarudiana tena.Baada ya kurudiana ndipo Kelvin

aliponieleza ukweli kwamba mwanamke aliyekuwa naye katika mahusiano ni mtoto wa hayati Rais mstaafu Malaki ambaye ndiye aliyekuwa mtunza fedha wa chama chetu.Alinieleza sababu ya kuachana naye ni kwamba siku moja usiku wakiwa hotelini,Rosana alipigiwa simu na mtu akatoka nje wakazungumza kwa takribani saa nzima.Kelvin alitaka kumfahamu mtu huyo aliyezungumza naye kwa muda mrefu namna ile ni nani,Rosana alidai ni rafiki

yake.Asubuhi wakati Rosana akiwa bafuni,Kelvin aliichukua namba ile ya simu iliyompigia Rosana usiku.Alimpa mmoja wa marafiki zake ambaye anafanya kazi katika kampuni moja ya simu amsaidie kuitafuta namba ile ni ya nani.Jibu alilolipata ni kwamba namba ile ya simu ni kutoka nchi moja huko Amerika.Kelvin aliendelea kufuatilia kumjua mtu anayeitumia namba ile ya simu.Rosana aligundua kile alichokuwa anakifanya Kelvin ukatokea ugomvi mkubwa

wakaachana.Hata baada ya kuachana,bado Kelvin aliendelea kutaka kumfahamu mtu yule aliyekuwa anawasiliana na Rosana.Siku chache kabla ya kutoweka kwake aliniambia kwamba amegundua mtu aliyekuwa akiwasiliana na Rosana anaitwa Benard Timothy.Alifanikiwa kuipata picha yake mtu huyo anafanana sana na hayati rais Malaki isipokuwa huyo Benard amekuwa na ndevu nyingi tofauti na Malaki.” Alinyamaza baada ya Ruby kuguna

“Du ! aliguna Ruby

“Siku tatu baada ya kufanikiwa kumpata Benard,Kelvin alianza kupokea vitisho kutoka kwa watu asiowafahamu.Alinifuata akaniambia kwamba ana hofu na maisha yake.Tuliifuatilia moja ya namba ya simu ambayo ilitumika kutoa vitisho vile tukagundua ni ya mmoja wa viongozi wa chama chetu.Kiongozi huyo wa chama alinifuata akaniambia nimuonye Kelvin asiendelee kulichimba kaburi lake mwenyewe.Sikuwahi

kumweleza maneno hayo ila nilimtaka aachane na kile alichokuwa anakifanya.Kelvin alisisitiza kuwa anataka kuthibitisha zile fununu kuwa Rais mstaafu Malaki yuko hai.Wiki moja baadae ndipo alipotoweka.Siku ile alipotoweka alipanga kunieleza kitu tutakapokutana usiku lakini hatukufanikiwa kukutana usiku.” Alisema Regina

“Nimeonana na Gavana usiku huu naye pia amenieleza kuwa siku chache kabla ya Kelvin kupotea alikuwa ni mtu

mwenye mawazo mengi sana.Inaonekana kilichokuwa kinamsumbua kichwa chake ni hilo suala” alisema Mathew

“Umeonana na Gavana? Aliuliza Regina

“Ndiyo nimeonana naye usiku huu” alijibu Mathew.

“Kitu gani kingine amekwambia? Aliuliza Regina.Mathew alimueleza kila kitu kuhusu mazungumzo yake na Gavana.

“Gavana bado anaamini kuna kitu unakifahamu

kuhusu kupotea kwa Kelvin.Hisia zake ni za kweli? Kuna kitu unakifahamu kuhusiana na tukio hilo? Aliuliza Mathew.Ilimchukua Regina muda kidogo kutafakari na kujibu swali lile.

“Gavana yuko sahihi ndiyo maana ananifuatilia” alisema Regina.

“Tueleze tafadhali kile unachokifahamu kuhusiana na tukio la kutoweka Kelvin.” Alisema Mathew

“Kuna siri moja ambayo bado watu hawaifahamu

kuhusu Kelvin.He was a deep undercover agent.”

“Alikuwa mpelelezi? Ruby aliuliza

“Ndiyo.Alikuwa akifanya kazi SNSA”

“Ulifahamu vipi kuhusu jambo hilo? Aliuliza Mathew.

“Tuliporudiana aliniomba msamaha.Ili kurudiana nilimpa sharti la kunieleza ukweli kwa nini aliniacha akaanzisha mahusiano na Rosana.Alinieleza ukweli lakini akaniomba iwe ni siri yangu

nisimueleze mtu.Alinieleza kila kitu kuhusu yeye kuwa ni mpelelezi.Aliniweka wazi kuwa kuanzisha mahusiano na Rosana ilikuwa ni moja ya misheni zake katika kuchunguza kuhusu tetesi za Rais mstaafu Malaki kuwa hai" alisema Regina

"Where is he? Mathew aliuliza

"Nani? Aliuliza Regina

"Kelvin.Where is he? Is he dead? Aliuliza tena Mathew

Regina alionekana kutokuwa tayari kujibu lile swali.

“Regina umeamua kueleza ukweli hivyo usisite tafadhali.Tueleze ukweli wote unaoufahamu.” Alisema Mathew.Dakika moja na sekunde kadhaa ilikatika Regina akiwa bado anatafakari.Hatimaye alifumbua mdomo na kusema

“He’s not dead” alinyamaza kidogo.Mathew na Ruby walikuwa kimya wakimsikiliza.

“Baada ya kugundua kuhusu mipango ya kutaka kumuua Kelvin aliamua kutoroka na kwenda mahali kusiko julikana.” Alisema Regina

“Unafahamu mahali aliko? Aliuliza Mathew

“Hapana sifahamu mahali alipo.Hakunieleza mahali anakoenda ila naamini yuko hai” alijibu Regina

“Rosana yuko hapa nchini? Aliuliza Mathew

“Rosana aliamua kuachana na siasa na hakuna anayefahamu mahali alipo hivi sasa” alijbu Regina ukapita ukimya kidogo.

“Kwa nini unataka kukimbilia Zales? Mathew aliuliza

“Nitakwenda wapi kujificha zaidi ya kwenda huko?Jeshi la polisi wananisaka hivi sasa kwa tuhuma za mauaji.Maisha yangu hapa tayari yameharibika.Ninataka

kwenda Zales kujificha” alijibu Regina.

“Ulimuahidi Innocent kumlipa fedha mara tu utakapofika Zales.Unategemea kutoa wapi fedha? Aliuliza Mathew

“Niliwaeleza kwamba nilipogundiua uwepo wa mfadhili wa chama nilipewa shilingi milioni mia moja kwa ajili ya kufunga mdomo.Niliambiwa nisiweke fedha hizo katika benki za hapa nchini kwani ningeanza kufuatiliwa mahali nilikotoa

fedha hizo.Nilisaidiwa kufungua akaunti ya siri huko Zales ambako nimekuwa nikitunza fedha zangu.Nina fedha nyingi huko.Ninataka kwenda kuanza maisha mapya huko" alisema Regina.

"Regina nakushukuru kwa kuamua kufunguka na kutueleza ukweli.Huna sababu ya kukimbia.Nimekwisha kuhakikishia kwamba sisi tupo na tutahakikisha kwa namna yoyote ile unakuwa salama.Tutahakikisha tunautafuta ushahidi wa kutosha ambao utakutoa

katika matatizo haya uliyonayo.” Alisema Mathew

“Mathew nimekuwa nikisikia simulizi zako na ninaamini haya uyasemayo lakini ninaomba mnisaidie niweze kuondoka hapa nchini kwenda nje ya nchi nikajifiche huko hadi pale mambo yatakapotulia.” Alisema Regina

“Regina pamoja na kwamba uko katika matatizo makubwa hivi sasa lakini nataka nikueleze ukweli kwamba kukimbia si suluhu ya

haya matatizo uliyonayo.Umesema bado una ndoto za kuwa mwanasiasa hivyo unatakiwa usimame imara upambane kuhakikisha unafikia ndoto zako.Taifa bado linawahitaji vijana kama ninyi.Hata hivyo kuna mambo ambayo unatakiwa uyarekebishe kama unataka kufika mbali kisiasa.Kitendo ulichokifanya cha kwenda kuficha hela nje ya nchi si kitendo kizuri.Mambo kama hayo hufanywa na mafisadi wanaoiba fedha katika nchi zao na kwenda kuzificha nje ya

nchi.Ninakuhakikishia kwamba suala hili litakwisha na pale litakapokamilika anza kurekebisha makosa yako na kitu cha kwanza unachotakiwa kukirekebisha ni hilo la fedha ulizozificha nje ya nchi.Unatakiwa uzirejeshe fedha hizo hapa nchini.” Alisema Mathew lakini Regina alibaki kimya hakujibu kitu

“Umenielewa Regina? Aliuliza Mathew

“Nimekuelewa Mathew lakini bado ninasisitiza kuondoka hapa nchini kwani

sintakuwa salama.Siwezi kuukimbia mkono wa dola.Hayo uliyonieleza ninakubaliana nayo lakini naomba mniruhusu niondoke nchini” alisema Regina

“Regina narudia tena hapa nchini hautaondoka.Utaendelea kukaa hapa na tutahakikisha unakuwa salama.Tutalimaliza hili suala.Kuendelea kusisitiza kuondoka nchini kunatufanya tuhisi kuna mambo mengine unayakimbia na si hili la tuhuma za mauaji” alisema Mathew

“Hakuna jambo lingine ninalolikimbia hapa nchini zaidi ya hilo la kubambikiwa kesi ya mauaji.Tayari upo mpango wa kuniangamiza hivyo kama nikikamatwa kwa namna yoyote ile utakuwa ni mwisho wangu.” Alisema Regina

“Ninalifahamu hilo ndiyo maana nilimwambia Innocent aendelee kutengeneza ile hati uliyomuomba ili pale nitakapojiridhisha kuwa upo ulazima wa kuondoka nchini basi mimi mwenyewe nitakusaidia kuondoka.”

Alisema Mathew.Regina alibaki kimya.

“Regina tunaelewana? Aliuliza Mathew

“Ndiyo.”alijibu Regina

“Good.Kwa mara nyingine tena ahsante kwa haya uliyotueleza.Yatatusaidia sana katika uchunguzi wetu.Kwa sasa nenda ukapumzike” alisema Mathew.Regina aliinuka akaeleka katika chumba chake.

“Mathew, haya aliyoyasema Regina

sikuyategemea kabisa.” Alisema Ruby

“Ni mambo mazito” alisema Mathew

“Nini mtazamo wako baada ya kumsikia Regina? Aliuliza Ruby

“Maelezo yake yametufumbua macho hasa kuhusu utata wa kifo cha Rais Malaki. Maelezo ya Regina yananishawishi niamini kwamba mzee Malaki yuko hai.Malaki ana hasira na chama alichokuwa anakiongoza hasa baada ya

kumkatalia kubadili katiba ili aongoze kwa muhula wa tatu.Anataka kukiondoa madarakani chama hicho ndiyo maana akaasisi chama cha Ukombozi wa Afrika kilichojimega kutoka chama cha Ukombozi ambacho alikianzisha kwa malengo ya kuudhoofisha upinzani nchini.Kwa sasa chama cha Ukombozi naweza kusema kimekufa kabisa.Chama kikuu cha upinzani kwa sasa ni chama cha ukombozi wa Afrika na ndicho kinachopanga kuvuruga uchaguzi mkuu

endapo mgombea wake hataibuka mshindi wa kiti cha Rais.Kwa haraka haraka ukilitazama jambo hili utaona huu ni mwendelezo wa hasira za mzee Malaki.” Alisema Mathew

“Unahisi Malaki ndiye mfadhili ambaye Regina hakubahatika kumfahamu? Aliuliza Ruby

“Sina uhakika huo lakini kuna kila dalili kwamba ndiye mfadhili wa chama ili kutimiza malengo yake.Jambo la pili hatukujua kama Kelvin ni

mpelelezi.Kwa kiasi kikubwa alikaribia kuufahamu ukweli kuhusu rais mstaafu Malaki kama yuko hai au alifariki dunia.Hapo ndipo alipoanza kupata vitisho kutoka kwa watu mbali mbali na hatimaye alitoweka na hadi sasa hajulikani mahali alipo.Hili nalo linanipa uhakika mkubwa kuwa Rais Mstaafu Malaki anaweza kuwa hai. Tutalifukua kaburi kujiridhisha je ni kweli alifariki dunia? Kama hakufariki yuko wapi? Kelvin naye yuko wapi? Hayo ni maswali ambayo hatuna budi

kuyatafutia majibu lakini bila kusahau jukumu la msingi la kubaini ni namna gani chama hicho cha ukombozi wa Afrika kimejiandaa kuvuruga uchaguzi mkuu.Tunatakiwa kulibaini hili haraka sana ni namna gani hawa watu wamejipanga.Vile vile tunatakiwa kumsaka Gosu Gosu mahali alipo.Usiku huu hakuna kulala ninakwenda tena kuonana na Gavana kumpa mrejesho wa haya niliyoyapata kutoka kwa Regina.” Alisema Mathew.Baada ya majadiliano

ya dakika chache Mathew akitumia simu ya Ruby alimpigia simu Gavana akamjulisha kuwa anataka kwenda kuonana naye usiku ule.Gavana alimkaribisha.Mathew alimuacha Ruby akaondoka kuelekea kwa Gavana.

“Mambo mapya yanazidi kuibuka na kulifanya jambo hili liwe kubwa zaidi.Kama iliyvo ada yangu hakuna jiwe litasalia juu ya jiwe.Nitalichimba jambo hili hadi mzizi wake.” Aliwaza

Mathew akiwa garini akielekea nyumbani kwa Gavana.

****

Papi Gosu Gosu bado alibaki katika mshangao kwa kile alichokishuhudia ndani ya kile chumba.

“This is not true” alirudia tena Gosu Gosu.

“It’s true Gosu Gosu”alijibu jamaa mmoja aliyekuwa amevalia suti nadhifu ya rangi ya bluu.Kichwani alikuwa amevalia kofia ya mzunguko

nayo ya rangi ya bluu.Pembeni ya kiti alichokuwa amekaa kulikuwa na fimbo maalum yenye nakshi za dhahabu.

“Karibu Gosu Gosu” alisema yule jamaa

“Bado siamini macho yangu.Joseph imekuaje uko hapa? Una mahusiano gani na hawa watu? Aliuliza Gosu Gosu akiwa katika mshangao.

“Nataka unijibu je uko pamoja na watu hawa? Aliuliza Gosu Gosu

“Gosu Gosu hukupaswa kulifahamu hili lakini imelazimu uletwe hapa ili uufahamu ukweli” alisema yule jamaa ambaye Gosu Gosu alimuita kwa jina la Joseph

“Joseph kitu kimoja tu ambacho ninahitaji kukifahamu ni je unashirikiana na hawa mashetani? Aliuliza Gosu Gosu.Sura yake haikuonesha masihara.Joseph alimtazama Gosu Gosu halafu akajibu.

“Sisi na hawa unaowaita mashetani ni mtandao

mmoja.” Alijibu Joseph.Sura ya Gosu Gosu ilizidi kujikunja kwa hasira.

“Kwa nini hukuniambia toka awali kama tunashirikiana na hawa watu? Unawafahamu vizuri hawa watu ni akina nani? Aliuliza Gosu Gosu.

“Gosu Gosu ili mipango yetu ikamilike lazima tushirikiane na hawa watu unaowachukia.Tunawahitaji sana.Nitakufafanulia wakati mwingine lakini kwa leo kuna jambo la muhimu ambalo

nataka tulizungumze” alisema Joseph.

“Duh ! siamini kama tumefikia hatua ya kushirikiana na hawa watu” alisema Gosu Gosu kwa sauti ndogo ikionesha kukata tamaa.

“Sikiliza Gosu Gosu.Ulitumwa kuifanya kazi muhimu sana kule Arusha.Kwa sababu unazozifahamu wewe uliamua kuiharibu ile kazi.Kitu ambacho hukifahamu ni kwamba ile kazi uliyotumwa kuifanya Arusha ina umuhimu

mkubwa sana katika mipango yetu.”alisema Joseph

“Uliufahamu mpango ule? Aliuliza Gosu Gosu kwa mshangao uliochanganyika na hasira

“Ndiyo.Ninafahamu kila kitu.Gosu Gosu uliposhindwa kuimaliza ile kazi uliyotumwa umetengeneza bomu ambalo linaweza kulipuka muda wowote na kuharibu mipango yetu yote.Kwa kuwa ni wewe uliyelitega bomu hilo unatakiwa ufanye kazi ya ziada kulitegua bomu hilo ili lisilete

madhara kwetu.” Alisema Joseph

“Una maanisha nini Joseph? Bomu gani nimelitega? Aliuliza Gosu Gosu

“Kuna mtu anaitwa Mathew Mulumbi.Huyu ni mtu hatari sana kwa mipango yetu.Ni wewe ndiye uliyesababisha Mathew akaenda Arusha na kuvuruga mipango yetu yote.Mtu yule ambaye ni swahiba wako mkubwa amekwisha nusa harufu ya jambo letu na ataifuatilia hadi ahakikishe

anafika katika chanzo cha harufu hiyo.Ni mtu asiyeshindwa lolote.Ni rafiki yako lakini kwetu sisi ni kiumbe mbaya sana sawa na Ziraili mtoa roho.Nataka kwanza nifahamu kwa nini uliamua kumjulisha Mathew kuhusu kile ulichotumwa kukifanya Arusha? Aliuliza Joseph.Gosu Gosu alikaa kimya kwa muda halafu akasema

“Wewe ndiye unayepaswa kuangushiwa mzigo wote wa lawama.” Alisema Gosu Gosu

akimtazama Joseph kwa macho makali sana.

“Ulipaswa kuniambia kama kile nilichotumwa kukifanya Arusha kina mahusiano na mipango yetu.Unafahamu walichokifanya hawa wajinga hadi kunilazimisha niende Arusha kufanya yale mauaji? Aliuliza Gosu Gosu.

“Ninafahamu kila kitu” alijibu Joseph na kumfanya Gosu Gosu azidi kukasirika.

“Kwa nini ukakubali mpango kama ule?

Unafahamu ni maumivu kiasi gani wamenisababishia washenzi hawa? Alifoka Gosu Gosu huku akiinuka

“Easy Gosu Gosu..Take it easy” aliomba Joseph.Gosu Gosu alisimama kwa sekunde chake akimtazama Joseph halafu akaketi.

“Joseph kwa mambo waliyonifanyia hawa watu nimekwisha weka ahadi nitawamaliza wote bila kujali kama wana umuhimu kwetu au hawana.Ninakuhakikishia nitaua moja baada ya

mwingine.Hiyo ni nadhiri nimeiweka na hata yule mwanamke Bernadetha nimekwisha mwambia kwamba kama wameshindwa kuniua wakati wanayo nafasi basi nikipata nafasi sintawaacha hai nitawamaliza wote.Ni watu makatili sana hawa.Ni kwa sababu yao nimemkosa mwanamke niliyempenda kuliko wote duniani" alisema Gosu Gosu na kunyamaza baada ya picha ya Ambola kumjia kichwani.Aliumia sana.

“Yule mwanamke shetani mkubwa aliamuru mwanae auawe nilipokataa kufanya alichotaka nikifanye.Kwa hilo sintomsamehe hata kidogo! Alifoka Gosu Gosu.Joseph alimtazama kwa muda halafu akasema

“Gosu Gosu kuna mambo mengi ambayo hujayafahamu bado.Nitakueleza japo kwa kifupi lakini kwa sasa nataka kwanza tulimalize lile ambalo nimekuitia hapa.” Alisema Joseph

“Nilikueleza kuhusu bomu hatari ulilolitengenza ambalo linakwenda kulipuka na kuhariu mipango yetu yote.Bomu hilo ni Mathew Mulumbi.Narudia tena huyu ni mtu hatari sana kwetu.Yule mwanamke uliyetumwa kwenda kumuua kule Arusha anafahamu mambo mengi na yuko katika harakati za kutaka kuvujisha siri hizo ndiyo maana ikaamriwa auawe yeye pamoja na yule mwenzake uliyemuua.Kwa sasa tunaamini mwanamke yule yuko na Mathew Mulumbi na

atamueleza kila kitu anachokifahamu.Hiyo ni sababu inayotufanya tumsake kwa udi na uvumba rafiki yako Mathew Mulumbi pamoja na yule mwanamke haraka sana.Ni wewe peke unayeweza kutusaidia kufahamu mahali aliko Mathew kwa sasa.Unafahamu sehemu zake zote za kujificha.Ninataka Mathew Mulumbi na yule mwanamke wauawe” alisema Joseph.Gosu Gou alimtazama kwa macho yaliyojaa hasira,akasimama.

“Wewe ni nani wa kuniamuru jambo kama hilo? Aliuliza Gosu Gosu.Joseph naye akasimama.

“Mimi kama kiongozi wako ndiye ninayekuamuru kwamba lazima Mathew Mulumbi auawe.Hakuna mwingine anayeweza kulifanikisha hilo zaidi yako Gosu Gosu.” Alisema Joseph kwa sauti kali kidogo.Kimya kifupi kilipita halafu akasema.

“Sikiliza Gosu Gosu,mambo yetu yanakwenda vizuri hadi

sasa.Mipango yetu ambayo tumeiandaa kwa miaka miwili sasa inakwenda kukamilika lakini ukamilifu wa mipango yetu yote unaanzia hapa Tanzania.Hiyo ni sababu nimeungana na hawa watu ambao unawaita mashetani.Kama Mathew Mulumbi akiharibu mipango ya hawa watu hapa Tanzania ni wazi hata mipango yetu itashindwa kufanikiwa" alisema Joseph.

"Joseph mbona sikuelewi? Aliuliza Gosu Gosu

“Hutanielewa kwa sasa lakini pale mambo yatakapoharibika ndipo utaamini maneno yangu.Gosu Gosu tumekaribia sana kufanikisha mpango wetu.Hatupaswi kukubali mpango wetu ukashindwa kufanikiwa kwa sababu ya mtu mmoja ambaye ni Mathew Mulumbi.Juhudi za kukushawishi kueleza mahali alipo Mathew Mulumbi zilipogonga mwamba ndipo nikaelekeza uletwe kwangu nizungumze nawe.Sina hakika

kama utasema hapana.” Alisema Joseph

“Joseph umenichanganya sana.Sikutegemea kusikia maneno haya kutoka kwako.Mimi katu siwezi kushirikiana na watu kama hawa hata kama wana msaada kwetu.” Alisema Gosu Gosu.

“Naomba uketi Gosu Gosu” alisema Joseph.Gosu Gosu alimtazama halafu akaketi.

“Nafahamu hasira zako ni kwa sababu ya kutenganishwa na mpenzi wako Ambola.Laiti

ungemfahamu Ambola ni nani usingeumiza kichwa chako.” Alisema Joseph

“Una maanisha nini? Aliuliza Gosu Gosu.

“Nitakueleza kidogo kuhusu Ambola” alisema Joseph.

KIGOMA – MIAKA 12 ILIYOPITA

Gari mbili aina ya Landcruiser V8 zote zikiwa na rangi nyeupe ziliwasili katika kambi waliyokuwa wakiishi wakimbizi kutoka jamhuri ya kidemokrasia ya Congo wilayani Kasulu.Kutoka ndani ya zile gari walishuka jamaa wanne ambao walipokelewa na moja wa viongozi wa kambi ile akawapeleka hadi katika ofisi yake.

“Karibuni” alisema yule mkuu wa kambi.

“Tunashukuru.Sisi si wakaaji sana.Tumekuja kuufuata ule mzigo kama uko tayari.” Alisema jamaa mmoja mfupi mnene ambaye alionekana kiongozi wa wale watu wanne.

“Kila kitu kimeandaliwa.” Alisema kiongozi wa kambi ambaye kibao kilichokuwa mezani kwake kilionesha aliitwa Jumanne Ndwale.Alifungua moja ya droo za meza yake akatoa bahasha ndogo iliyokuwa na picha mbili za wasichana.

“Huyu wa kwanza ana miaka kumi na mbili.Anaitwa Ambola Kabembo.” Alisema Jumanne.

“Huyu unafahamu ametokea sehemu gani ya Congo? Aliuliza yule jamaa mfupi mnene.

“Nimejaribu kuzungumza naye lakini hataki kabisa kuzungumza chochote kuhusiana na wapi alikotokea.”

“Huyu mwingine anaitwa nani?

“Huyu jina lake Maria ana miaka minne.Huyu aliokotwa njiani na majeshi ya Afrika akaletwa hapa.Hatuna taarifa zake kamili na hawezi kujileza vyema” alijibu Jumanne.

“Tunashukuru sana Jumanne kwa msaada huu” alisema yule jamaa mfupi akaingiza mkono katika mfuko wake wa koti akatoa bahasha iliyotuna akamkabidhi Jumanne ambaye bila kuifungua aliiweka katika mfuko wake wa koti halafu akatoka mle ofisini baada ya dakika kadhaa akarejea akiwa

ameongozana na wasichana wawili.

“Ambola mtaongozana na hawa watu,mnakwenda kuishi uraiani” alisema Jumanne.

“Hawa ni akina nani? Aliuliza Ambola

“Hawa ni watu kutoka serikalini,wamekuja kuwachukua wewe na Maria mmepata kibali cha kuondoka kambini na kwenda kuishi maisha mazuri uraiani” alisema Jumanne.

Ambola na Maria ambao hawakuwa na mizigo yoyote waliongozana na wale watu hadi katika gari wakaondoka pale kambini.Kutoka Kasulu safari ilikuwa ya moja kwa moja hadi Kigoma mjini ambako walifikia katika hoteli moja kiubwa.Pale walikutana na mwanamama aliyejitambulisha kwao kama Mama Bernadetha.

“Ambola na Maria kuanzia sasa mtaishi na huyu mama.Ni mtu mwema hana tatizo lolote.Amekubali kwa moyo

mmoja kuishi nanyi.” Alisema yule jamaa mfupi mnene.

Usiku wa siku ile Bernadetha aliwafuata akina Ambola chumbani kwao akawaambia kuanzia siku ile wataanza kutumia majina mapya.Ambola ataitwa Ambola Perfect na Maria utatumia jina la Elizabeth Perfect.Wamesajiliwa kama ndugu.Hawatajulikana kama raia wa Congo bali watanzania.Wazazi wao Perfect Lyimo na Bernadetha Lyimo.” Alisema Bernadetha

na kumuonesha kila mmoja cheti chake cha kuzaliwa.

Siku iliyofuata walipanda ndege wakaelekea Dar es salaam ambako walianza maisha mapya.Bernadetha na mume wake ambao hawakubahatika kupata mtoto waliwalea na kuwatunza akina Ambola kwa mapenzi makubwa.Ambola alipotimiza miaka kumi na nane alifanyiwa sherehe ndogo katika mojawapo ya hoteli kubwa.Baada ya sherehe kumalizika yeye na Elizabeth walikutana na mtu anaitwa

Meja Adam Muzinga.Huyu aliwahi kuwa mwanajeshi katika jeshi la Congo.Adam aliwaeleza sababu ya kukutana nao.

“Nimekuja kuzungumza nanyi kwa kuwa sasa ninyi ni wasichana wakubwa na mnaweza kuelewa kile nitakachowaeleza.”alisema Meja Adam

“Ninaitwa Meja Adam Muzinga.Nimekuwa mwanajeshi katika jeshi la Congo lakini kwa sasa ninaishi nchini Afrika kusini.Mimi ni

kiongozi wa mtandao wa siri wa wakongomani walioko nje ya nchi yetu ambao tunajipanga kurejea nchini kwetu na kuikomboa kutoka katika mikono ya wanyonyaji.Tunataka kwenda kumaliza uasi unaoendelea nchini kwetu.Tunaamini nchi yetu ikiwa na amani itapiga hatua kubwa kutokana na utajiri mkubwa wa rasilimali ambazo kwa sasa haziwanufaishi wakongo.Mipango hii tumeianza muda mrefu kwa kuwaandaa vijana ambao

tutashirikiana nao katika mpango huo.Ninyi ni sehemu ya mpango huo.” Alisema Adam na kuwatazama akina Ambola

“Mpango huo ni mzuri na binafsi ninauunga mkono.Mimi na mwenzangu sote tunafahamu athari za machafuko yanayoendelea nchini Congo.Ni kwa sababu ya machafuko hayo sote tumewapoteza ndugu zetu.Hata hivyo sisi tayari ni raia wa Tanzania hatuwezi kuwa na msaada wowote

katika mpango huo.” Alisema Ambola

“Ninyi kuwa watanzania ni sehemu ya mpango.Tulitaka muishi uraiani bila hofu ili iwe rahisi kutoa msaada pale itakapohitajika.Si ninyi tu wako wenzenu wengine pia ambao tumewasambaza nchi mbalimbali ” Alisema Adam

“Ni msaada gani ambao sisi tunaweza kuutoa? Aliuliza Ambola

“Ambola kwa kuwa wewe tayari umetimiza miaka kumi na nane tutafanya mpango ili

upelekwe katika mafunzo.Baada ya kutoka mafunzoni utaelekezwa nini cha kufanya” alisema Adam

****

Maelezo yale ya Joseph kuhusu Ambola yalimuacha Gosu Gosu katika mshangao mkubwa.

“Hivyo ndivyo ilivyokuwa Gosu Gosu.Wakati Ambola akiwa mafunzoni,Meja Adam Muzinga aliuawa hivyo nilikabidhiwa nafasi

yake.Nilipokuja hapa Tanzania kwa mara ya kwanza nikiwa na Rais wa Congo aliyemaliza muda wake nilikutana nawe.Nilikueleza mipango yetu na ukakubali kujiunga nasi.Wakati mipango yetu ikiendelea ilibainika kwamba yule mwanamke Regina kuna mambo aliyafahamu .Baada ya kumfuatilia kwa muda wenzetu wa hapa Tanzania ambao tunashirikiana nao walijiridhisha kwamba Regina ana mpango wa kuvujisha siri hivyo njia pekee ya kuzuia mipango yao isivuje ni kwa

kumuua.Namna ya kumuua ilileta shida kidogo ndipo nilipowapa wazo la kukutumia wewe.”

“Kwa nini mimi? Aliuliza Gosu Gosu

“Tuliamua kumtumia mtu ambaye hata kama mambo yakiharibika basi anayo sehemu ya kukimbilia.Kama mambo yakiharibika hapa Tanzania unaweza ukakimbilia Congo ndiyo maana tukakuchagua wewe.Sababu nyingine ninakufahamu vizuri uwezo wako katika kutumia

silaha.Ninaamini kabisa ungelimaliza jambo hilo bila kuacha alama zozote kwa jeshi la polisi kumpata muuaji.Hakuna namna ambayo ungeshawishiwa ukakubali kufanya mauaji hayo ndiyo maana mara tu aliporejea Ambola kutoka mafunzoni alitumwa kuanzisha mahusiano nawe.Lengo la kuanzisha mahusiano nawe lilikuwa ni kuandaa tukio lile lililotokea ambalo Bernadetha alilitumia kukulazimisha uende Arusha kufanya yale mauaji.”

“Aaaggghh ! alipiga ukelele Gosu kwa hasira.

“Huo ndio ukweli Gosu Gosu.Ilibidi kumtumi Ambola ili ukaifanye ile kazi kule Arusha.” Aliongeza Joseph.

“Joseph kwa nini ukanifanyia hivi? Kwa nini mkacheza na akili yagu kiasi hiki? Aliuliza Gosu Gosu kwa hasira

“Kama nilivyokueleza kwamba ilibidi itumike njia hii kukulazimisha uende Arusha kufanya yale mauaji.Bila kutumia njia hii usingekubali

kwenda huko” alijibu Joseph.Bado Gosu Gosu aliendelea kumtazama kwa macho yaliyojaa hasira.

“Nimeumia sana Joseph kwa hiki mlichonifanyia.Kulikuwa na ugumu gani kuniita na kunitaka nikafanye ile kazi kuliko kumtumia Ambola? Tayari nilikwisha zama mapenzini naye.Nilikuwa nafikiria hata kumvisha pete ya uchumba kumbe hakukuwa na mapenzi yoyote kati yetu.Ulikuwa ni uongo mtupu ! alifoka Gosu Gosu

“Hakukuwa na mapenzi yoyote.Ambola alikuwa kazini.Bila yeye usingekubali kuifanya ile kazi kule Arusha.” Alisema Joseph.Kimya kilitawala mle chumbani.

“Where is she? Aliuliza Gosu Gosu.Joseph hakujibu .

“Nakuuliza Joseph Ambola yuko wapi? Is she dead? Aliuliza

“Hapana hajafa.Ambola ni mzima kabisa.Ule ulikuwa ni mpango wa kukutisha ili ukubali kueleza mahali alipo Mathew Mulumbi.Kuanzia

sasa fahamu kuwa Ambola si mtoto wa Bernadetha wala yeye na Elizabeth hawana undugu wowote wa damu” alisema Joseph.Gosu Gosu aliutazama mkono wake wa kulia kwa hasira halafu akamtazama Joseph.

“Joseph ninatamani nichane kifua chako niutoe moyo wako niutafune .Ulichonitendea ni kitendo kibaya mno na cha kikatili ! alisema Gosu Gosu lakini Joseph hakuwa na wasiwasi wowote

“Gosu Gosu ninakufahamu vizuri sana.Ninafahamu unaweza ukafanya hicho unachokisema lakini hayo yote hayana msaada kwetu kwa sasa.Kazi kubwa tuliyonayo hivi sasa ni kuhakikisha tunalimaliza tatizo lililojitokeza ambalo ni wewe uliyelisababisha.Tatizo hilo ni Mathew Mulumbi.Naomba nikuweke wazi Gosu Gosu kwamba ili mipango yetu iende vizuri lazima kuhakikisha wenzetu hapa Tanzania mambo yao yanakwenda vizuri.Sisi na wao

tumeungana.Kama wakifanikiwa kumuingiza mtu wao kushika nafasi ya Rais,huyo ndiye atakayetusaidia na sisi kufanikisha mipango yetu lakini kama wenzetu wakishindwa basi hata sisi itatuwia ugumu kufanikisha mipango yetu.Hukupaswa kuyafahmu haya yote lakini kwa hatua iliyofikia hivi sasa imenilazimu nikueleze ukweli wote ili ujue hatari tuliyonayo.” Alisema Joseph.Gosu Gosu hakumjibu chochote alikuwa kimya kabisa

“Gosu Gosu ninafahamu Mathew Mulumbi ni mtu wako wa karibu sana ambaye kwa maelezo uliyowahi kunipa ndiye aliyefanikisha ukafika hapa ulipofika leo.Ni mtu unayemuhesabu kama ndugu yako lakini ukweli utabaki ule ule kwamba Mathew ni mtanzania na wewe ni mkongomani.Ninyi ni marafiki tu hamna undugu wowote wa damu.Haya ni mapambano ya kuikomboa nchi yetu.Tumekwisha kula kiapo iwe jua iwe mvua lazima tuhakikishe tunaikomboa nchi

yetu.Kwa sasa yupo mtu ambaye anatishia mipango yetu kutokufanikiwa ambaye ni Mathew Mulumbi.Huyu ni kirusi mbaya ambaye kama hatadhibitiwa haraka atasababisha mipango yetu yote ambayo tumeiandaa kwa muda mefu kushindwa kufanikiwa.Tafadhali ninakuomba kama ndugu yako tuoneshe mahali alipo Mathew Mulumbi.Wewe unafahamu sehemu zake zote za kujificha.Tuna uhakika mkubwa Mathew yuko na Regina na kadiri

tunavyochelewa kumpata ndivyo tunavyozidi kujiweka katika hatari kwani atazifahamu siri zote alizonazo Regina za kuhusu mipango yetu.Kama kweli una nia ya dhati ya kuikomboa nchi yetu basi kitu cha kufanya kwa sasa ni kumuondoa Mathew Mulumbi" alisema Joseph.Gosu Gosu alionekana kuumiza kichwa kutafuta jibu la kumpa Joseph.

"Gosu Gosu ninakuacha kwa dakika chache nataka utafakari kwa kina juu ya jambo hili na nitakaporejea

utanipa jibu kama uko tayari kuendelea na mipango yetu” alisema Joseph akainuka na kutoka mle ndani.

“Nimepitia nyakati nyingi ngumu katika maisha yangu lakini sijawahi kuwa na wakati mgumu kama huu.Ugumu si kwa sababu ya Ambola.Japo nimeumia lakini yule ni mwanamke tu ninaweza kumpata mwingine.Ugumu si kwa sababu ya mauaji niliyoyafanya.Ugumu ni kutakiwa kumuua Mathew Mulumbi.Yule ni ndugu yangu.Ndiye aliyeniokota

kutoka mavumbini akanifikisha hapa nilipofika leo.Ninajuta kukutana na Joseph kwani kama si yeye nisingekuwa hivi sasa na wakati mgumu kama huu.” Aliwaza Gosu Gosu

“Mathew Mulumbi ni mzalendo wa kweli kwa nchi yake.Tanzania imekuwa ni nyumbani kwetu.Ni katika ardhi hii ya Tanzania ndipo nimejifunza nini maana ya maisha.Starehe zote nimezifahamu nikiwa hapa Tanzania.Ninaishi kwa amani hapa.Si mimi tu bali mamia ya

wakimbizi bado wanaishi hapa na wengine tayari wamekwisha pewa uraia wa nchi hii.Hii nchi ndiyo kimbilio letu ambao tunatoka katika nchi zenye kukumbwa na vurugu na machafuko ya mara kwa mara.Nilipokubali kuungana na Joseph katika kile kinachoitwa mpango wa kuitoa Congo katika mikono ya mabeberu,niliamini mpango huo utakuwa a manufaamakubwa sana kwa nchi ya Congo lakini hiki nilichokifahamu leo kimenishtua sana.Sikutegemea

kabisa kusikia eti tunashirikiana na akina Bernadetha. Kuna kitu amekizungumza Joseph kwamba kufanikiwa kwa mipango yetu kunategemea na kufanikiwa kwa wenzetu ambao ni akina Bernadetha.Kuna kitu masikio yangu yalikisikia kutoka kwa Joseph kwamba kama wenzetu wakifanikiwa kumuweka rais madarakani basi na sisi tutakuwa tumefanikiwa mipango yetu.Nini wanapanga kukifanya katika mpango wao wa kumuweka huyo rais wao

madarakani? Nguvu kubwa inatumika hivi sasa kumtafuta Regina ambaye inasemekana amezifahamu siri za mipango yao.Ni siri zipi hizo alizogundua Regina? Hapa kuna mambo mazito yanayoendelea.Huu mtandao tayari umenipa wasiwasi mkubwa.Ni mtandao hatari sana na wanachopanga kukifanya ni kitu kibaya sana kwa nchi hii iliyotamalaki amani.Nchi hii imebarikiwa kupata viongozi wa kipekee kabisa ambao wanachaguliwa kidemokrasi hivyo

haiwezekani ukafanyika ujanja ujanja kumuingiza madarakani mtu ambaye si chaguo la wananchi.Nimesimama njia panda sijui nielekee upande upi.Niendelee kushirikiana na hawa wenzangu katika mipango yao ya Congo mpya au nisimame upande wa Tanzania? Alijiuliza Gosu Gosu akasimama na kuweka mkono mmoja ukutani.

“Mimi kwa sasa ni raia wa Tanzania hata kama nina damu ya Congo.Mathew Mulumbi amenifundisha kuwa mzalendo kuipenda nchi

hii hata kama itanigharimu uhai wangu.Nimeshiriki katika misheni mbali mbali nikiwa na Mathew kwa ajili ya usalama wa nchi hii.Hapana siwezi kukubali hujuma yoyote ikafanywa hapa nchini.Nitaungana na akina Mathew katika kuumaliza mtandao huu wenye mipango miovu dhidi ya Tanzania hata kama itanibidi kuwasaliti wenzangu" aliendelea kuwaza

"Nadhani nitakuwa nimefanya maamuzi sahihi kabisa japo nitakuwa nimejiingiza katika hatari

kubwa lakini niko tayari kwa lolote.Nitamlinda Mathew Mulumbi kwa gharama zozote zile.Kuanzia sasa natakiwa kuonekana niko upande wao na nikubali kufuata maelekezo wanayoyatoa.Hapa itanilazimu kukubali mpango wa kumuua Mathew Mulumbi.Lengo hapa ni kuifahamu mipango waliyonayo.Nitaanza kwanza kwa kumchimba Joseph anieleze kuhusu mipango waliyonayo akina Bernadetha.Kila taarifa nitakayoipata nitatafuta namna ya kuifikisha kwa akina

Mathew ambao nina uhakika hadi hivi sasa watakuwa kazini wakifanyia uchunguzi suala lile la kutaka kumuua Regina.” Aliwaza na kwenda tena sofani akaketi.

“Habari ya Ambola nayo imenishtua na kunisikitisha mno.Sikutegemea kabisa mwanamke kama yule ambaye nilimpenda kwa dhati ya moyo wangu,mwanamke mwenye mikono laini na sauti tamu ya kuvutia, kumbe ni nyoka.Kinachoniumiza zaidi Ambola alionesha mapenzi mazito kwangu nikiamini

ndiye mwanamke anayenifaa kumbe ni Chui asiye na madoa.Natamani nikutane na Ambola ana kwa ana japo sifahamu nini kitatokea ikionana naye.Nayakumbuka maneno ya Mathew siku moja aliwahi kunionya nisiwaamini sana wanawake hawa warembo.Kila mwanamke mrembo niliyewahi kuwa naye aliniacha na maumivu.Nadhani sina bahati katika mambo ya mapenzi.Mambo haya niwaachie akina Mathew wenye nyota zao.” Aliwaza

Gosu Gosu na kutolewa mawazoni baada ya mlango kufunguliwa akaingia Joseph.

“Gosu Gosu naamini umetumia muda huu mfupi kutafakari kuhusu mipango yetu.Nini maamuzi yako? Aliuliza Joseph .Gosu Gosu alivuta pumzi ndefu akasema

“Nimetafakari kwa kina sana maneno yako.Kwa upande Fulani nimejiona mjinga.Nchi yangu inapaswa kuwa mbele ya kitu chochote.Kama ulivyosema kuwa Mathew ni rafiki yangu

lakini yeye atabaki mtanzania na mimi nitabaki mkongomani. Ukombozi wa taifa langu ni muhimu sana kuliko urafiki wangu na Mathew.Kwa mantiki hiyo basi niko tayari kuongoza zoezi la kumsaka Mathew Mulumbi.” Alisema Gosu Gosu

“Ninakufahamu Gosu Gosu ndiyo maana nikaamuru uletwe kwangu tuzungumze.Ninafurahi umekubali kufanya jambo la muhimu.Hata hivyo nataka unieleze kile kilichotokea kule Arusha.Ilikuaje ukaharibu ile

kazi muhimu? Mathew Mulumbi aliingiaje katika misheni yetu? Nieleze kila kitu kilivyokuwa tafadhali nataka kujua" alisema Joseph.Zilipita sekunde kadhaa Gosu Gosu akasema

"Mchezo wote wa Bernadetha kunilazimisha niende Arusha kufanya mauaji unaufahamu hivyo sina haja ya kuelezea, hapa nitakueleza kile kilichotokea nikiwa Arusha" alisema Gosu Gosu na kumuelezea Joseph kile kilichotokea jijini Arusha.Hakuficha kitu

alimueleza namna mambo yote yalivyokwenda hadi alivyowasiliana na Mathew Mulumbi.

“Niliambiwa nikatoe roho ya mtu ambaye simfahamu wala sijui amefanya kosa gani hivyo nilikuwa na shauku ya kutaka kumfahamu mtu yule ni nani na kwa nini ameuawa ndiyo maana nikawasiliana na Mathew ili anisaidie kujua mtu yule ni nani.Ninawalaumu sana kwa kutonieleza ukweli.Kama ungenieleza ukweli kabla sijakwenda Arusha haya yote

yasingetokea.” Alisema Gosu Gosu akaendelea kumueleza Joseph kile kilichoendelea baada ya kuwasiliana na Mathew na hadi alivyoshindwa kumuua Regina .

“Kwa mara nyingine ninakuangushia wewe zigo la lawama kwa kunificha ukweli.Kama ungenieleza ukweli kuanzia mapema kuwa Regina anapaswa kuuawa nisingesita kuizinga ile bunduki na kumfumua kichwa chake.Nilisita kumuua si kwa sababu alikuwa meza moja na Mathew Mulumbi bali

sikufahamu sababu ya kwa nini auawe?Nilitaka Mathew Mulumbi achunguze na ajue sababu kwa nini Regina anatakiwa kuuawa.” Alisema Gosu Gosu akanyamza kwa muda.

“Hivyo ndivyo ilivyotokea kule Arusha.Nakubali nilifanya kosa lakini sote tunapaswa kubeba lawama.Ninyi ndio mnaopaswa kulaumiwa zaidi kwa sababu mlinificha ukweli.”

“Gosu Gosu nimekuelewa vizyuri.Nashukuru kwa kunieleza ukweli.Nakubali sote

tulikosea na kusababisha mambo kuharibika.Hata hivyo tunatakiwa kurekebisha makosa yaliotokea na kuanzia sasa tutazingatia sana suala la uwazi.Makosa tutayarekebisha kwa kuhakikisha Mathew Mulumbi na Regina wanaondolewa.Katika hilo tunakutegemea sana wewe" alisema Joseph

"Mimi niko tayari kuongoza zoezi la kuwasaka Mathew Mulumbi na Regina ambao naamini wako pamoja hivi sasa.Ninafahamu maficho yake.Lakini kabla sijanyanyua

mguu wangu kwenda kuanza zoezi hilo ninataka kuufahamu ukweli kuhusu hawa akina Bernadetha.Kwa nini umewaamini kiasi cha kushirikiana nao?" aliuliza Gosu Gosu

"Gosu Gosu suala hili ni pana kidogo lakini nitakueleza kwa ufupi ili upate walau picha kwa nini tunashirikiana nao." Alisema Joseph na kunyamaza kimya kwa muda kidogo.

"Misheni yetu ni kuikomboa nchi yetu ya Congo.Hatuwezi kufanikiwa

misheni hii bila kupata uungwaji mkono mkubwa ndiyo maana tunashirikiana na wenzetu hawa akina Bernadetha.Hawa wenzetu lengo lao ni kuhakikisha mtu wao wanayemuunga mkono anashinda katika uchaguzi wa Rais unaotarajia kufanyika hivi karibuni hapa Tanzania.Kufanikiwa kwao ndio kufanikiwa kwetu kwa sababu kwa mujibu wa makubaliano yetu ni kwamba mtu wao akishinda urais ndiye atakayetusaidia kwa hali na mali kuhakikisha tunaiondoa

madarakani serikali iliyoko sasa nchini Congo.Kwa ajili hiyo basi hatuna budi kuhakikisha tunawasaidia wenzetu kufanikisha mpango yao ili na wao watusaidie mipango yetu.” Alisema Joseph

“Unadhani mtu wao atafanikiwa kushinda uchaguzi? Aliuliza Gosu Gosu

“Wanao uhakika mkubwa kwani kila kitu ni mipango tu.Nisingepoteza muda wangu kushirikiana nao kama nisingejua kuna manafaa

makubwa tutayapata” alisema Joseph

“Tanzania ili ugombee urais lazima uwe na chama.Hawa watu tunaoshirikiana nao ni chama kipi? Aliuliza Gosu Gosu.

“Gosu Gosu unauliza maswali mengi naomba uniamini kwamba mashirikiano haya yana faida kubwa kwetu”

“Ninalifahamu hilo lakini ninataka na mimi niwafahamu hawa watu tunaoshirikiana

nao ni watu wa aina gani.” alisema Gosu Gosu

“Hawa watu wanamuunga mkono mgombea kutoka chama kimoja kati ya vyama vya siasa vilivyosimamisha wagombea katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.Usiniulize ni chama gani kwa sababu hata mimi mwenyewe sifahamu.” Alisema Joseph

“Tunatakiwa kumfahamu mgombea wanayemuunga mkono ili tujue kama ana

nguvu ya kushinda uchaguzi au vipi” alisema Gosu Gosu.

“Kushinda uchaguzi si lazima uwe na nguvu bali ni mbinu tu.Usiwe na hata chembe ya shaka Gosu Gosu mgombea huyo anayeungwa mkono na hawa wenzetu anakwenda kushinda uchaguzi mkuu mwaka huu” alisema Joseph.

“Unaweza ukaniambia ni mbinu zipi ambazo zitatumika kumfanya huyo mgombea ashinde uchaguzi? Aliuliza Gosu Gosu

“Hata mimi sifahamu ni mbinu zipi zitatumika lakini nimehakikishiwa kwamba mtu wao lazima atashinda na akishinda basi misheni yetu imefanikiwa”

“Ni vipi kama huyo mgombea hatashinda uchaguzi? Aliuliza Gosu Gosu

“Hilo haliwezi kutokea.Kwa mikakati ambayo nimeambiwa imewekwa mgombea huyo lazima ashinde kwa namna yoyote ile hata kama damu itamwagika.”

“Unapozungumzia kumwaga damu una maanisha nini? Vurugu? Mapinduzi? Aliuliza Gosu Gosu

“Gosu Gosu namna yoyote ile ambayo itamuingiza mgombea huyo ikulu sisi haituhusu.Tunachohitaji ni yeye ashinde ili na sisi mambo yetu yakae vizuri.” Alisema Joseph

“Joseph tunapaswa kuwa makini na kuifahamu mipango yote ya hawa jamaa.Mingine inaweza ikatuweka hata sisi katika matatizo.”

“Usihofu Gosu Gosu hawa watu ni mtandao mkubwa wenye nguvu hapa nchini.Usidhani Bernadetha yuko mwenyewe.Yeye ni mtu mdogo sana katika huo mtandao”

“Vigogo gani wako katika mtandao huo? Aliuliza Gosu Gosu

“Gosu Gosu hatuwezi kukaa hapa tukiulizana maswali wakati Mathew Mulumbi hatujui mahali alipo.Naomba tulishughulikie kwanza hili la Mathew na

tukifanikiwa kumuondoa ninakuahidi nitakujibu maswali yako yote unayohitaji kuyafahamu.Kwa sasa naomba tafadhali nifuate” alisema Joseph huku akiinuka na Gosu Gosu akamfauat nyuma.

****

“Bwana Mathew karibu sana.Umenipa hofu kidogo kwa ujio wako usiku huu.Kulikoni? aliuliza Gavana wakati akimkaribisha Mathew nyumbani kwake.

“Samahani Gavana kwa usumbufu lakini imenilazimu nije tena kwako usiku huu” alisema Mathew

“Kuna nini bwana Mathew? Aliuliza Gavana.Bado uso wake ulionesha wasiwasi

“Mzee nimekuja kwako kuna mambo muhimu yamenileta.Ni kuhusiana na suala la Kelvin” alisema Mathew na kunyamaza akamtazama mzee yule aliyekuwa na hofu kubwa mara baada ya jina la mwanae Kelvin kutajwa.

“Umepata nini kuhusu Kelvin? Aliuliza Gavana

“Kelvin alikuwa anafanya kazi gani? aliuliza Mathew

“Alikuwa meneja wa benki moja binafsi.Alikuwa pia na biashara nyingine kama kampuni ya utalii,mashamba na vyombo vya usafiri” alijibu Gavana.Mathew alimtazama kwa muda kidogo halafu akauliza.

“Ulifahamu kama mwanao ni mpelelezi?

Swali lile lilimshtua sana Gavana.

“Mpelelezi?

“Ndiyo.Aliwahi kukwambia au unalifahamu hilo?

“Hapana.Mwanangu hajawahi kuwa mpelelezi”

“Alikuwa mpelelezi.” Mathew alisema na kimya kikatawala.

“Kelvin ni mwanangu lakini vile vile alikuwa rafiki yangu.Mimi naye kuna baadhi ya mambo tulielezana bila

kufichana.Kama angekuwa mpelelezi angeniambia.” Alisema Gavana.

“Kuna mambo mengine asingethubutu kukwambia.Alikuwa mpelelezi wa siri wa idara ya siri ya usalama wa wa nchi kifupi SNSA.”

“SNSA? Gavana alishangaa

“Ndiyo”

“Una hakika bwana Mathew? Aliuliza Gavana

“Nina uhakika”

“Nimeshangaa kwa sababu ninaifahamu idara hiyo na mkurugenzi wake bwana Faraji Dilele ni rafiki yangu mkubwa.Hapa nyumbani amekuwa akifika mara kwa mara.Ni yeye aliyenifahamisha kuhusiana na uwepo wa idara hiyo ya siri ya usalama wa ndani wa nchi.Hata siku moja hajawahi kuniambia kwamba mwanangu ni mmoja wao.” Alisema Gavana akionekana kushangaa.

“Tuliweke hilo pembeni kwa muda.Nimefanikiwa kupata mambo kadhaa kuhusu

Kelvin na sababu ya kutoweka kwake” alisema Mathew na kumueleza Gavana yale mambo yote aliyoelezwa na Regina.

“Hii taarifa mbona imeniogopesha sana.Kwa mtazamo wako baada ya kugundua mambo haya,unadhani Kelvin yuko hai?Aliuliza Gavana

“Uwezekano wa Kelvin kuwa hai ni mkubwa japo hakuna anayejua mahali alipo” alijibu Mathew.

“Nini mipango yako baada ya kuyagundua haya? Kuna mipango yoyote ya kutafuta na kujua mahali alipo Kelvin? Aliuliza Gavana

“Baada ya kuzipata taarifa hizi niliona itakuwa vyema nije kwanza nikupe mrejesho usiku huu huu ili upate picha ya kile kinachoendelea” alisema Mathew.

“Ninakushukuru sana Mathew kwa kuniletea taarifa hii.Nimefarijika kiasi japo bado kiza kimetanda kuhusu

mahali alipo Kelvin.” Alisema Gavana.

“Mzee katika maongezi yako ulisema mkurugenzi wa SNSA ni rafiki yako”alisema Mathew

“Ndiyo ni rafiki yangu sana.Hapa nyumbani hufika mara kwa mara.”

“Ingekuwa vizuri tukaonana naye na kupitia kwake tutaweza kupata taarifa za kina kuhusu Kelvin na kazi aliyokuwa anaifanya.Kuna uwezekano SNSA wakafahamu

mahali alipo Kelvin.” alisema Mathew

“Nitazungumza naye kesho ili tupange kuonana jioni hapa kwangu”alisema Gavana

“Hatuwezikusubiri hadi kesho.Tunatakiwa kuonana naye usiku huu” alisema Mathew

“Usiku huu? Aliuliza Gavana akishangaa

“Ndiyo.Usiku huu huu tunatakiwa kuonana naye.Zungumza naye tafadhali mwambie kuna jambo la

dharura aidha aje hapa au tumfuate kwake” alisema Mathew.

“Kwa sasa ni usiku sana Mathew.Watu wamepumzika.Kwa nini tusisubiri hadi kesho? Aliuliza Gavana

“Mzee hakuna kusubiri kesho.Kila kitu lazima kifahamike usiku huu huu.Ushauri mwingine kama utampigia simu usitumie simu yako tumia ya mkeo” alisema Mathew.Gavana aliinuka akaenda chumbani kwake

halafu akarejea akiwa na simu mbili akaandika namba ya Faraji katika simu ya mke wake akapiga.Baada ya muda ikapokelewa.

“Mheshimiwa Gavana” alisema Faraji Dilele

“Mkurugenzi.Habari za usiku huu.Samahani kwa usumbufu huu mkubwa” alisema Gavana

“Bila samahani mheshimiwa Gavana.Nimeshtuka kwa simu yako ya usiku huu wa manane.Si kawaida yako

kupiga simu muda kama huu” alisema Faraji.

“Ni kweli mkurugenzi.Sijawahi kupiga simu muda kama huu lakini nimelazimika kupiga leo.Nina jambo la dharura limetokea” alisema Gavana

“Jambo gani? Kuna usalama huko? Aliuliza Faraji kwa sauti yenye wasiwasi.

“Faraji hatuwezi kuzungumza katika simu.Nahitaji kuonana nawe”

“Usiku huu? Aliuliza Faraji.

“Ndiyo usiku huu”

“Kuna nini mheshimiwa Gavana? Aliuliza Faraji

“Nitakueleza tukionana .” Alisema Gavana.Faraji alivuta pumzi ndefu halafu akauliza.

“Unataka tuonane wapi? Aliuliza Faraji.

“Tukutane hapa kwangu tafadhali” alisema Gavana

“Sawa ninakuja hapo sasa hivi” alisema Faraji.

Baada ya kukata simu,Gavana alimgeukia Mathew akamtazama kwa macho ya mshangao.

“Mathew Mulumbi” alisema Gavana.

“Naam mzee”

“Nimekuogopa.Haya uliyonileta usiku huu sikuyategemea kabisa.Nimetumia fedha nyingi kutafuta ukweli kuhusu mwanangu lakini sikuwahi kupata chochote hadi wewe ulipokuja kunifumbua macho usiku huu.Kuna picha

nimeipata kufuatia haya uliyonieleza.Baada ya jeshi la polisi kuthibitisha kuwa Regina hahusiki katika tukio la kupotea Kelvin, nilikata tamaa kabisa lakini ni Faraji aliyenipa moyo kwamba uchunguzi zaidi unatakiwa kufanywa kuhusu tukio lile na ndiye aliyenishauri nitumie wapelelezi wa kujitegemea.Sikujua kwa nini Faraji alisisitiza kuwa lazima uchunguzi ufanywe kumbe kuna kitu alikuwa anakifahamu.” Alisema

Gavana huku akiendelea kumtazama Mathew

“Atakapokuja atatueleza kila kitu.Ndiyo maana nikasisitiza lazima tuonane naye usiku huu” alisema Mathew.Gavana alimuacha Mathew akaenda kumuamsha mkewe ili awatengenezee kahawa .

****

Gosu Gosu na Joseph waliingia katika chumba ambamo kulikuwa na watu

wanne.Mmoja wa watu hao alikuwa ni Bernadetha.Gosu Gosu alimkata jicho kali sana.

“Karibu uketi Gosu Gosu” alisema Joseph.

“Nimezungumza na Gosu Gosu.Nimempa picha ya kile kinachoendelea hivi sasa na amekubali kuongoza zoezi la kumsaka Mathew Mulumbi.” Alisema Joseph.

“Gosu Gosu hivi sasa ni usiku mwingi hakuna haja ya kuendeleza mjadala zaidi.Tunachohitaji ni kitu kimoja tu ambacho ni kujua

mahali alipo Mathew Mulumbi.Wewe unafahamu sehemu zake zote ambazo anaweza akapatikana” alisema Bernadetha.Gosu Gosu alivuta pumzi ndefu halafu akasema

“Kabla sijawaeleza chochote nataka tuelewane.Nimezungumza na Joseph amenieleza mambo kadhaa.Tumegundua kosa lilikuwa wapi hadi tukafika hapa tulipofika.Kosa kubwa lililofanyika lilikuwa ni ukosefu wa uwazi.Mlificha mambo hadi tumefika hapa.Sikujua kama ninyi ni

wenzetu tunashirikiana. Kama mngenifahamisha angali mapema haya yote yasingetokea .Ninachowaomba kuanzia sasa tuzingatie uwazi.Tusifichane mambo” alisema Gosu Gosu

“Tumekuelewa Gosu Gosu.Hilo litazingatiwa” alisema Bernadetha.Baada ya sekunde kadhaa Gosu Gosu akaendelea.

“Mathew Mulumbi ni mtu mwenye kuchukua tahadhari kila wakati.Anafahamu amezungukwa na hatari za

mara kwa mara hivyo kila wakati huwa katika tahadhari kubwa.Ili kujihakikishia usalama,Mathew amekuwa na kawaida ya kujenga nyumba katika sehemu mbali mbali za jiji kwa ajili ya kujificha pale anapokuwa katika hatari.Sehemu ya kwanza ya kumtafuta Mathew ni jijini Arusha.Tunatakiwa kujiridhisha kama bado yuko Arusha au amekwisha ondoka.Kama hayupo Arusha basi hakuna sehemu nyingine anakoweza kwenda zaidi ya

Dar es salaam.” Alisema Gosu Gosu

“Unafahamu mahali alikofikia jijini Arusha? Aliuliza Bernadetha.Gosu Gosu aliwaelekeza hoteli ambayo Mathew alifikia jijini Arusha.Bila kupoteza muda Bernadetha alimpigia simu kamanda wa polisi mkoa wa Arusha akamuelekeza kufuatilia katika ile hoteli alikokuwa amefikia Mathew kama bado yupo .

“Inaonekana huu mtandao ni mkubwa sana.Hadi

kamanda wa polisi mkoa wa Arusha naye yumo” aliwaza Gosu Gosu.

“Wakati tunaendelea kusubiri jibu kutoka Arusha,nataka utuelekeze sehemu ambazo Mathew Mulumbi huzitumia kujificha” alisema Bernadetha.

“Kuna sehemu tatu ambazo ni muhimu sana kwa Mathew na ambazo huzitumia kujificha” alisema Gosu Gosu

“Tunataka kuzifahamu sehemu hizo tafadhali” alisema Joseph

“Kwa maelekezo ya mdomo itakuwa vigumu kufika mahali hapo.Ninatakiwa kufika hapo mimi mwenyewe” alisema Gosu Gosu

“Gosu Gosu tunahitaji maelekezo ya mahali hapo sisi utatuma vijana wetu watakwenda wewe bado utaendelea kuwepo ndani” alisema Bernadetha.Gosu Gosu alimtazama kwa macho makali.

“Nilisema hapo awali kwamba kama mnataka tuendelee kwenda mbele

lazima tuaminiane.Kama mimi nanyi ni kitu kimoja kwa nini mnashindwa kuniamini? Alifoka Gosu Gosu

“Gosu Gosu bado hatuna imani nawe kutokana na kile ulichokifanya kule Arusha.Wewe ndiye uliyetufikisha hapa tulipofika baada ya kumkaribisha Mathew Mulumbi katika mipango yetu.Itachukua muda kukuamini tena ndiyo maana tunataka utuelekeze sehemu ambazo Mathew hujificha.Tutatuma vijana wetu watakwenda kuifanya

kazi ya kummaliza Mathew Mulumbi.” Alisema Bernadetha.

“Jamani suala hili mimi na Gosu Gosu tumekwisha lizungumza na kulimaliza.Gosu Gosu ndiye pekee tunayemtegemea kwa sasa hivyo basi tunatakiwa kutumia busara kubwa” alisema Joseph.Gosu Gosu alisimama akamtazama Bernadetha

“Hakuna yeyote humu anayemfahamu Mathew Mulumbi zaidi yangu.Yule ni

kiumbe wa ajabu.Mnadhani mnaweza kumuua Mathew Mulumbi kwa kutumia vijana wenu hawa dhaifu? Mnajidanganya sana.Mimi pekee ndiye ninayeweza kuwasaidia namna ya kumuua Mathew Mulumbi.Ni mimi pekee ambaye ananiamini hivyo basi kama mnataka kummaliza niacheni niingie kazini" alisema Gosu Gosu

"Gosu Gosu usihofu kuhusu watu wa kuifanya hiyo kazi.Tunachohitaji ni kujua mahali anakojificha Mathew .Mambo mengine tuachie sisi

tutajua namna ya kuyamaliza” alisema Bernadetha.

Gosu Gosu aliwaelekeza katika nyumba mbili ambazo huzitumia Mathew Mulumbi kujificha pale anapokuwa katika hatari.Wakati Gosu Gosu akiendelea kutoa maelekezo,Bernadetha alipigiwa simu na kamanda wa polisi mkoa wa Arusha ambaye alimjulisha kuwa Mathew hakuwepo katika hoteli aliyokuwa amefikia jijini humo.

“Mathew amekwisha ondoka katika ile hoteli alikofikia jijini Arusha.Hii ni ishara kuwa tayari yuko hapa Dar es salaam.Tutayatumia maelekezo ya Gosu Gosu kutuma vijana wetu kwenda katika sehemu hizo ambazo anaamini Mathew anaweza kuwa amejificha” alisema Bernadetha

“Ni vijana wa aina gani ambao mnataka kuwatuma kwenda kumsaka Mathew Mulumbi? Aliuliza Gosu Gosu.

“Usihofu.Tunacho kitengo maalum ambacho kinashughulika na masuala kama hayo” alijibu Bernadetha kwa kifupi.

“Baada ya hapa nini hatima yangu? Aliuliza Gosu Gosu.

“Utakuwa huru pale Mathew Mulumbi na Regina watakapouawa” alijibu Bernadetha.Watu wanne waliingia ndani ya kile chumba Gosu Gosu akawatazama kwa jicho la shari.

“Gosu Gosu tafadhali” alisema Joseph baada ya kuusoma uso wa Gosu Gosu.

“Mpelekeni akapunzike.” Bernadetha aliwaambia wale watu.Gosu Gosu aliongozana nao kwenda katika moja ya chumba ndani ya nyumba ile.

“Hawa watu wamejipanga vilivyo.Nitahakikisha ninaufahamu mtandao wao wote na malengo yao kwa taifa hili.Nina uhakika mkubwa mahali nilikowaelekeza hawatampata Mathew.Yule mtu huwa harudii kujificha

sehemu moja mara mbili.Nina uhakika lazima watakuja kunitafuta watakapomkosa” aliwaza Gosu Gosu akiwa ndani ya kile chumba kizuri akipumzika

****

Faraji Dilele mkurugenzi wa idara ya siri ya usalama wa nchi aliwasili nyumbani kwa Gavana.

“Ninashukuru sana Faraji kwa kufika.Samahani pia kwa

usumbufu huu mkubwa” alisema Gavana.

“Usijali mheshimiwa Gavana” alijibu Faraji.Gavana alimuongoza hadi katika chumba cha mazungumzo.Faraji alishangaa kidogo baada ya kukuta kuna mtu mwingine ndani ya kile chumba.

“Karibu Faraji.” Gavana alimkaribisha Faraji.Mathew Mulumbi alisimama ili asalimiane na Faraji.

“Faraji kutana na Mathew Mulumbi” alisema Gavana na

kumtazama Faraji usoni alionesha mshangao.

“I know this guy” alisema Faraji

“You know him? Aliuliza Gavana

“Yes .I know him.How’re you Mr Mathew Mulumbi? Nimefurahi kukutana nawe ana kwa ana” alisema Faraji.

“Mimi pia nimefurahi kuonana nawe Mr Faraji.” Alisema Mathew wakapeana mkono.

“Ninyi watu mnafahamiana? Aliuliza Gavana

“Nimelisoma faili la Mathew Mulumbi nikiwa bado katika shirika la ujasusi Tanzania.Nimefurahi leo kukutana naye ana kwa ana” alisema Faraji.

“Mathew, huyu ndiye bwana Faraji Dilele.”alisema Gavana

“Nimefurahi kukutana naye” alisema Mathew.Faraji aliinuka sofani akavua koti lake.

“Nimeanza kuhisi joto baada ya kumkuta Mathew Mulumbi ndani ya hiki chumba usiku huu.Nina hisi hiki si kikao cha kawaida” alisema Faraji na Gavana akatoa kicheko kidogo.

“Ni kweli kikao hiki cha usiku wa manane si cha kawaida.” Alisema Gavana

“Hivi vinaitwa vikao vya wanga” alisema Faraji aliyeonekana ni mtu mcheshi sana.Wote wakaangua kicheko.

“Mheshimiwa Gavana nimeitika wito wa usiku wa manane.Nini kinaendelea hapa? Aliuliza Faraji.

“Faraji nimekuita hapa kuna mambo muhimu ya kuzungumza.Kubwa ni suala la Kelvin.Bado sijakata tamaa kama ulivyonishauri.Kama unakumbuka yule mpelelezi wa pili alinipa picha kuwa Regina kuna kitu anakifahamu kuhusu kutoweka kwa Kelvin.Nilimpata mpelelezi wa tatu anaitwa Johnson Kumbi kutoka Zambia.Nilimtuma Arusha kumfuatilia Regina

lakini usiku huu nimeletewa taarifa kuwa ameuawa.” Alisema Gavana

“Naye ameuawa? Faraji alishangaa sana

“Ndiyo ameuawa.”

“Gavana hapa kuna kitu.Haiwezekani wapelelezi watatu wote wauawe kabla hawajafika mbali katika upelelezi wao.Taarifa hizo umezipata wapi? Aliuliza Faraji

“Nimejulishwa na Mathew Mulumbi”

“Mathew alimfahamuje ? Alijuaje kama ana mahusiano nawe? Aliuliza Faraji.

Mathew alimueleza Faraji kisa chote namna Johnson alivyouawa na Gosu Gosu.Alimueleza pia kuhusu uchunguzi walioufanya hadi wakagundua alikuwa na mawasiliano na Gavana.

“Nani hawa wanaofanya mauaji haya na kwa lengo gani? aliuliza Faraji

“Baada ya kufahamu kuwa Johnson ameuawa, nilimuomba Mathew anisaidie

kufanya uchunguzi kuhusiana na suala la Kelvin.Usiku huu amekuja na taarifa ambayo imenilazimu nikuite hapa.Kabla sijakueleza chochote nataka unithibitishie je Kelvin alikuwa ni mpelelezi wa siri wa SNSA? Aliuliza Gavana.Faraji alionesha mshtuko.

“Kelvin? Aliuliza Faraji

“Ndiyo.Alikuwa mfanyakazi wa siri wa idara yenu? Aliuliza tena Gavana.Faraji alishindwa

kujibu alibaki anamtazama Gavana.

“Taarifa hiyo umeipata wapi? Aliuliza Faraji.

“Mheshimiwa Faraji,mimi ndiye niliyemletea Gavana taarifa hiyo.Nimeipata kutoka katika vyanzo vyangu vya kuaminika.Tunataka ututhibitishie hilo ili tuendelee na mambo mengine” alisema Mathew

“Faraji, Kelvin ni kama mwanao.Kama kweli unafahamu alikuwa anafanya kazi SNSA nieleze tafadhali”

alisema Gavana.Kilipita kimya kifupi Faraji akasema

“Ni kweli.Kelvin alikuwa mpelelezi wa siri wa SNSA” alisema Faraji

“Kwa nini hukuwahi kuniambia jambo hilo Faraji? Aliuliza Gavana

“Kelvin alikuwa katika wale wapelelezi wa siri sana ambao tunawahifadhi mno wasijulikane.Utanisamehe Gavana kwa kutokufahamisha kuhusu suala hilo” alisema Faraji

“Faraji ahsante kwa kutueleza ukweli.Ulifahamu jambo lipi alikuwa analichunguza kabla ya kutoweka kwake? Aliuliza Mathew

“Ndiyo ninafahamu.Alikuwa anachunguza fununu za Rais mstaafu Malaki Mnambara kuwa hai”

“Alikupa taarifa yoyote kuhusiana na uchunguzi aliokuwa anaufanya? Aliuliza Mathew

“Aliniambia amekaribia sana kuufahamu ukweli na aliahidi angenipa jibu baada ya wiki moja lakini alitoweka ghafla hivyo sikuweza kupata taarifa yoyote na sijui aligundua nini” alisema Faraji

“Mlifanya uchunguzi kuhusiana na kupotea kwake? Mligundua nini?Aliuliza Mathew

“Kuna jambo lilitokea baada ya Kelvin kupotea.Niliondolewa kazini bila kupewa sababu.Niliambiwa

nitapangiwa kazi nyingine lakini mpaka leo hii bado sijapangiwa kazi yoyote.Kuna tetesi nimezipata kutoka kwa watu wa karibu na Rais kuwa ana mpango wa kuniteua kuwa balozi.Kwa sababu hiyo mpaka leo hii sifahamu nini kinachoendelea kuhusiana na kupotea kwa Kelvin kwa sababu si mkurugenzi tena wa SNSA”

“Nani mkurugenzi wa sasa wa idara hiyo? Aliuliza Mathew

“Nimeambiwa anaitwa Julius Mukoke.” Alijibu Faraji

“Unapata picha gani ya wewe kuondolewa kazini muda mfupi baada ya Kelvin kupotea?Unahisi uchunguzi aliokuwa anaufanya ni sababu ya kukuondoa kazini? Aliuliza Mathew

“Ninahisi inaweza kuwa sababu.Kuna mambo mengi yanajitokeza kuhusiana na kutoweka kwa Kelvin ndiyo maana nilimshauri rafiki yangu Gavana kuwa uchunguzi

ufanyike ili kuupata ukweli” alisema Faraji

“Kelvin alikuwa mpelelezi wa siri,kuna mtu yeyote aliyefahamu kama alikuwa anachunguza suala la utata wa kifo cha Rais mstaafu Malaki? Aliuliza Mathew

“Ndiyo.Idara ya SNSA iko chini ya Rais hivyo kila siku lazima kuwasilisha kwake taarifa ya kila kinachoendelea ndani ya SNSA.Kila uchunguzi unaofanyika lazima aufahamu na lazima ajue kila mfanyakazi amepangiwa majukumu

yapi.Hivyo alifahamu fika kuwa Kelvin anachunguza utata wa kifo cha Rais mstaafu Malaki.”

“Aliwahi kutoa maoni yoyote kuhusiana na uchunguzi huo? Mathew aliuliza

“Kitu alichokishauri ni umakini mkubwa kwa sababu suala lile ni kubwa na zito.”

“Nataka kufahamu kuhusu SNSA na chama cha ukombozi.Nini mahusiano yenu? Aliuliza Mathew

“Kuna mahusiano baina ya SNSA na chama cha ukombozi lakini sina hakika kama bado mahusiano hayo yanaendelea kwa sababu chama cha ukombozi ni kama tayari kimekufa.Wakati wa utawala wa Rais Malaki alitupa sisi SNSA kazi ya kuchunguza nguvu ya vyama vya siasa hapa nchini na katika uchunguzi wetu tulibaini vyama vya siasa vilikuwa na nguvu kubwa.Baadhi ya vyama hivyo vilikuwa vinafadhiliwa fedha kutoka nje ya nchi.Rais mstaafu Malaki aliamua

kuunda chama cha siasa ambacho kitakuwa na nguvu kubwa lengo likiwa ni kuvidhoofisha vyama vingine vya siasa.SNSA tulipewa kazi hiyo na tulianzisha chama hicho.Licha ya kuwa na jukumu la msingi la kudhoofish vyama pinzani lakini chama hicho pia kilitumika kama sehemu ya SNSA kwani kupiitia makachero wetu tuliokuwa tumewapandikiza tuliweza kufahamu mikakati mbali mbali ya vyama vya siasa na kuhakikisha haifanikiwi.Hayo

ndiyo yalikuwa mahusiano ya SNSA na chama cha ukombozi.” Alijibu Faraji huku Mathew akimsikiliza kwa makini sana

“Nini kilitokea na kupelekea hadi chama cha ukombozi kupotea katika ramani? Mathew aliuliza lengo lake likiwa ni kuhakiki yale aliyoelezwa na Regina.

“Ninavyofahamu sababu kubwa ya kupasuka kwa chama cha ukombozi ni mgogoro ulioanza ndani ya chama tawala.Rais Malaki

alitaka kubadili katiba ili agombee urais kwa kipindi kingine cha tatu.Chama chake hakikumuunga mkono katika hoja yake hiyo.Baada ya kumalizika kipindi chake ndipo chama cha Ukombozi kilipomeguka na kikazaliwa chama cha ukombozi wa Afrika.Huo ukawa mwanzo wa chama cha ukombozi kudhoofika na kupotea kabisa katika ulingo wa siasa" alisema Faraji

"Unadhani Rais mstaafu Malaki anahusika katika

kudhoofika kwa chama cha ukombozi? Aliuliza Mathew

“Tetesi zinaeleza hivyo kuwa Malaki ndiye muasisi wa chama cha ukombozi wa Afrika lakini sina hakika kwa sababu sijawahi kufanya uchunguzi kulithibitisha hilo na wala yeye mwenyewe hakuwahi kujitokeza hadharani akadai kuunga mkono chama hicho” alijibu Faraji

“Unazungumziaje tetesi za Rais mstaafu Malaki kuwa hai? Mathew aliuliza

“Ninapenda tetesi kwa sababu ndizo hutupelekea kufanya uchunguzi na wakati mwingine kuibua mambo mazito.Tetesi hizi si za kupuuza hata kidogo.Yawezekana kuna ukweli ndani ndani yake na hasa ukichangia na suala la kutoweka kwa Kelvin.” Alijibu Faraji.

“Faraji nimekuuliza maswali hayo ili kulinganisha majibu yako na kile nilichokuwa nimekipata katika uchunguzi wangu wa awali.Majibu uliyonipa

hayajapishana na kile nilichokipata.Kwa kuongezea katika suala hilo la utata wa Rais mstaafu Malaki kuwa hai ni kwamba Kelvin alifanikiwa kuwa na mahusiano na binti wa Rais huyo mstaafu aitwaye Rosana ambaye alikuwa mtunza fedha wa chama cha ukombozi wa Afrika.Lengo lilikuwa kumchunguza binti huyo.Kelvin alibaini Rosana alikuwa na mawasiliano ya mara kwa mara na mtu mmoja ambaye baada ya kufuatilia namba yake aligundua mtu huyo alitokea nchi moja huko

Amerika.Alifanikiwa kuipata picha ya mtu huyo anafanana sana na Rais mstaafu Malaki lakini yeye jina lake ni Benard Timoth.Baada ya kufika hatua hiyo Kelvin alianza kupokea vitisho kutoka kwa watu mbali mbali na ghafla akatoweka.Kelvin alikaribia kuupata ukweli na akagundulika .Kuna siri kubwa katika suala hili la Rais mstaafu Malaki. ” alisema Mathew akanyamaza kidogo.

“Mambo haya umeyapata wapi? aliuliza Faraji

“Haya yote nimeyapata kutoka kwa Regina ambaye alikuwa mpenzi wa Kelvin” alisema Mathew

“Unamuamini Regina?Yule ni mwanamke ambaye hapaswi kuaminiwa kabisa.Nimepata taarifa zake anasakwa na jeshi la polisi kwa mauaji” alisema Faraji

“Regina anatafutwa na watu wanaotaka kumuua” alisema Mathew

“Nani wanataka kumuua? Taarifa zake zimesambaa kila mahali kuwa anatafutwa kwa

mauaji aliyoyafanya Arusha” alisema Faraji

“Ni kweli anatafutwa lakini hakuhusika katika yale mauaji.Hakuua kama inavyodaiwa na jeshi la polisi.Yeye ndiye alitakiwa kuuawa” alisema Mathew

“Hakuua? Aliuliza Faraji

“Hapana hakuua.Nilikuwepo wakati mauaji yale yanatokea na mimi ndiye niliyemuokoa Regina asiuawe” alisema Mathew na kuanza kumueleza Faraji

namna alivyoweza kumuokoa Regina.

“Nimeshangaa sana.Sikujua kama mambo yako hivyo.Watu hao ni akina nani waliopanga haya mambo? Nini sababu ya kutaka kumuua Regina? Aliuliza Faraji

“Bado tunawatafuta watu hao” alisema Mathew na kumueleza Faraji kile alichoelezwa na Regina kuhusu harakati za chama cha ukombozi wa Afrika kuhakikisha mgombea wao anashinda uchaguzi mkuu.

“Hizi taarifa una uhakika nazo? Unamuamini huyo Regina? Aliuliza Faraji

“Ndiyo ninamuamini.” Alijibu Mathew.

“Tangu kuanzishwa kwake sikuwahi kukiamini hiki chama cha ukombozi wa Afrika.Mmekwisha fahamu ni namna gani wanapana kuhujumu uchaguzi mkuu na kuhakikisha mgombea wao anashinda uchaguzi? Aliuliza faraji.

“Tunaendelea bado na uchunguzi.” Alisema Mathew

“Gavana hili jambo ni zito sana.Hili si jambo la kupuuzia hata kidogo.Lazima lifanyiwe kazi haraka sana kuhakikisha mipango hiyo haifanikiwi.Huu lazima ni mtandao wa vigogo wakubwa ambao wanashirikiana na chama hicho cha ukombozi wa Afrika kuhakikisha wanahujumu uchaguzi mkuu.” Alisema Faraji

“Ndiyo maana nimekuita hapa.Vijana hawa wanahitaji msaada ili waweze kufanikisha uchunguzi wao” alisema Gavana

“Natamani sana kama bado ningekuwa SNSA .Ile ni idara kubwa.Ina mtandao mpana sana.Wanao uwezo wa kufuatilia mawasiliano yote hapa nchini.Wanaweza kupata taarifa yoyote kutoka katika idara na taasisi zote za serikali.Wameunganishwa na kamera zote za ulinzi zilizo sehemu mbali mbali hapa nchini.Kwa ujumla SNSA wanaweza kumfuatilia mtu yeyote hapa nchini.Kwa bahati mbaya siko tena SNSA” alisema Faraji

“Tunahitaji sana kutumia mfumo wa SNSA katika uchunguzi huu.Kuna watu muhimu ambao tunahitaji kuwafuatilia lakini itakuwa rahisi sana kwetu kama tutatumia mifumo ya SNSA.” Alisema Mathew.

“Kwa sasa siwezi kuingia ndani ya ofisi ya SNSA.Nilipoondolewa katika nafasi yangu nilinyang’anywa kila kitu.Kadi yangu ambayo ndiyo funguo ya kuniruhusu kuingia ofisini,simu na kila kitu chenye mahusiano na idara hiyo.Hapa nilipo sina

hata mawasiliano na mtu yeyote wa SNSA kwa sababu wana mfumo wao maalum wa mawasiliano.” Alisema Faraji.

“Tafuta namna Faraji.Tunatakiwa kuunganisha nguvu kuhakikisha mipango hiyo miovu kwa nchi yetu haifanikiwi.Kwa namna yoyote ile hatuwezi kukubali kikundi kidogo cha watu wakapanga nani awe rais wa nchi kwa ajili ya maslahi yao wenyewe.Lazima tuhakikishe hilo halitokei” alisema Gavana

“Inavyoonesha jambo hili lina mkono wake pia kutoka nje ya nchi hivyo tutakaporuhusu mipango ya hawa jamaa ikafanikiwa tutakuwa tumewaruhusu mabeberu kuingia nchini na kufanikisha mipango yao.Kwa kuwa tayari tumefanikiwa kuifahamu mipango yao ni jukumu letu kuhakikisha mipango hiyo haifanikiwi.Hili lazima tulifanikishe kwa gharama zozote zile.Faraji kama una namna yoyote unayoweza ukatusaidia kuingia katika mfumo wa

SNSA tafadhali fanya hivyo.Usiogope kitu.Haya ni mapambano kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama” alisema Mathew.

Faraji alifikiri kwa muda halafu akasema

“Kuna kitu nimekumbuka.SNSA wana vituo vitatu vyenye mitambo yao ya mawasiliano hapa Dar es salaam.Kituo kimoja kipo kule Mzimu tete.Kutokana na hitilafu za mara kwa mara zilizokuwa zinatokea katika kituo hicho ambazo

zilihusishwa na imani za kishirikina kuwa eneo hilo kuna mizimu mikali, ilibidi kujenga kituo kingine na hicho kiliachwa kama akiba.Naweza kusema ni kituo kilichosahaulika kwa sababu hakuna anayekizungumza tena. Tunaweza kutumia kituo hicho kwani bado kimeunganishwa na mfumo wa SNSA lakini tunahitaji kuwa na mtu ambaye ni mtaalamu kutoka ndani ya SNSA.Bahati mbaya s……..” Hakumaliza sentensi yake Mathew akamkatisha.

“Tunaye bingwa wa mambo hayo ya elektroniki.Ni mdukuzi mbobezi.Anaweza akaifanya hiyo kazi kwa ufanisi mkubwa.Tuoneshe mahali kilipo hicho kituo” alisema Mathew

“Itabidi kazi hiyo ifanyike kesho.Ni sehemu ya hatari si rahisi kufika huko usiku huu.Ni mlimani halafu njia ya kufika huko ni ngumu inabidi kuacha gari chini ya mlima na kupita ndani ya msitu wenye mauza uza mengi.” Alisema Faraji

“Hatusubiri hadi kesho.Tunakwenda usiku huu huu.” Alisema Mathew

“Mathew niamini nikwambiavyo.Mahali hapo ni sehemu ya hatari sana usiku huu” alisema Faraji.Mathew alimtazama akasema

“Ninazipenda sehemu kama hizo za hatari.Tunakwenda usiku huu huu.” Alisema Mathew

“Faraji hakuna namna.Vijana wanataka kufika mahali hapo usiku huu hivyo

lazima uwapeleke”alisema Gavana

“Sijakataa kuwapeleka lakini ninapafahamu mahali hapo ni sehemu hatari kwa usiku huu.Itakuwa vyema kama tukienda huko kesho” alisema Faraji.

“Hatutasubiri hadi kesho.Tutakwenda huko usiku huu huu.Wenzetu hawalali wanapanga mipango ya kuhujumu uchaguzi mkuu hivyo nasi hatupaswi kulala.Tutafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha mipango

yao yote haifanikiwi” Alisema Mathew

“Faraji vijana wanataka kufanya kazi.Wapeleke mahali hapo” alisema Gavana.

“Usihofu hiyo mizimu wala kitu chochote.Nitakulinda”alisema Mathew.Faraji alimtazama Mathew kwa hofu.

“Yuko wapi huyo mwenzako? Aliuliza Faraji

“Tukitoka hapa tutakwenda kumchukua kisha

tutaelekea huko Mzimu tete” alisema Mathew

“Basi hakuna kupoteza muda.Safari ianze mara moja kwani muda unakwenda kasi sana” alisema Gavana huku akiitazama saa yake.Faraji na Mathew waliingia garini wakaondoka kuelekea katika makazi ya akina Mathew ili kumchukua Ruby.

****

Iliwachukua saa moja na dakika kadhaa kufika katika msitu wa Mzimu tete.

“Kutokea hapa hakuna njia ya gari kupanda mlimani hivyo tutaacha gari na kupanda mlimani kwa miguu” alisema Faraji.Mathew aliliingiza gari katika majani marefu wote wakashuka milango ikafungwa safari ikaanza kuelekea mlimani kilipo kituo cha mawasiliano cha SNSA.Mathew akiwa na begi la mgongoni ambalo lilisheheni vifaa mbali mbali ambavyo

Ruby alivihitaji,aliongoza njia kuelekea mlimani.

Walikatisha kati kati ya msitu wa kutisha.Sauti mbali mbali za vitu vya kutisha zilisikika.Ilikuwa ni safari yenye kuogofya sana.Faraji Dilele jasho lilimtoka.Ilikuwa ni safari ya kimya kimya kila mmoja akimuomba Mungu kwa imani yake ili wafike salama wanakoenda.

Walikutana na kijito ambacho daraja lake lilikuwa ni mti ulioanguka.Mti ule ulikuwa na utelezi mwingi

ishara kuwa ni muda mrefu hakuna watu wanaopita mahali pale.Walivuka kijito kile safari ikaendelea huku Faraji akitoa maelekezo.

Iliwachukua zaidi ya dakika hamsini kufika katika kituo walichokuwa wanakwenda.Kulizungushwa uzio imara wa waya.Kulikuwa na kiza totoro.Hakukuwa na dalili za kuwepo mtu mahali pale palipotisha.

“Ulisema kuna mlinzi mahali hapa? Aliuliza Mathew

“Nakumbuka kulikuwa na mlinzi ambaye alikuwa akilinda mitambo iliyopo hapa.Sina hakika kama bado panaendelea kulindwa.” Alisema

“Hakuna dalili za kuwepo mtu hapa.Liko wapi geti la kuingilia ndani? Mathew aliuliza.

“Njia ya kuingilia iko upande ule wa nyuma” alisema Faraji aliyekuwa anahema haraka haraka.

“Tuongoze tafadhali katika huo mlango” alisema Mathew.

Akiwa na hofu kubwa Faraji aliwaongoza akina Mathew kuelekea katika mlango wa kuingilia katika kituo kile.Walipita katika majani marefu huku Faraji akianguka zaidi ya mara tatu.

Waliufikia mlango wa kuingilia katika kituo kile ambao ulikuwa na kufuli mbili kubwa ambazo zilijaa kutu.Mathew alivua begi alilokuwa amelivaa mgongoni akatoa vifaa vyake vya kufungulia vitasa na makufuli.Ndani ya muda mfupi alifanikiwa kuyafungua

makufuli yale mawili.Waliingia ndani.Njia haikuonekana kutokana na majani yaliyotanda kila kona.Faraji aliwaongoza kuelekea katika jengo lililokuwepo katika kituo kile.Lilikuwa ni jengo la wastani kutumiwa kama ofisi ya watu wanne.Walihakiki kwanza eneo lile kuhakikisha hakuna mtu.

“Inaonesha ni muda mrefu tangu mtu alipofika mahali hapa” alisema Mathew.Alikichokonoa kitasa mlango ukafunguka wakaingia ndani.Mathew alimulika kwa

kutumia kurunzi yake.Aliuona mlango.

“Ule mlango ni wa nini? Aliuliza Mathew

“Kile ndicho chumba chenye kila kitu” alisema Faraji.Mathew aliusogelea mlango ule akaufungua akaingia ndani.Nyaya na mitambo mbali mbali vilisambaa katika kile chumba. Mathew alishangaa baada ya kuona vitaa vingi vidogo vidogo vikiwaka katika mle ndani,akamuita Faraji.

“Umeme wa kuendeshea vifaa vya hapa unatoka wapi? Aliuliza Mathew

“Umeme ulichukuliwa kutoka kijiji jirani ukapitishwa chini.Kabla ya umeme kutoka kijijini kufika hapa umeme uliokuwa unatumiwa ni wa nguvu ya jua” alisema Faraji.Mathew alimulika ukutani akaipata sehemu ya kuwashia taa akajaribu kuwasha taa ikawaka halafu akaizima.

“Hatupaswi kuwasha taa kwani mwangaza ukionekana

mahali hapa unaweza ukazua maswali mengi” alisema Mathew.Ruby aliingia katika kile chumba chenye mitambo yote.

Wakati Ruby akianza kazi yake ya kuhakikisha wanaingia katika mfumo wa SNSA Mathew alimtaka Faraji wazungukie mahali pale.

Mnara mrefu wa mawasiliano ulizungukwa na majani mengi.Sehemu nyingi kulikuwa na majani ikionekana ni muda mrefu tangu shughuli yoyote

imefanyika mahali pale.Kulikuwa na kijumba kidogo kilichokuwa na mlango imara wa chuma.

“Nyumba hii ni kwa ajili ya nini? Aliuliza Mathew

“Niliambiwa kuna wakati iliwahi kuwa nyumba ya jenereta lakini liliondolewa” alisema Faraji.Mathew alilishika kufuli akalifungua wakaingia ndani.Kati kati ya kile chumba kulikuwa mfuniko wa mbao.Mathew aliufungua mfuniko ule na kushuhudia shimo refu.Alimulika ndani ya

shimo lile ikaonekana mifupa ya watu na mafuvu kadhaa

“Unaona kule chini kuna nini? Mathew alimuuliza Faraji ambaye alishtuka sana baada ya kuiona mifupa ile ya binadamu ndani ya shimo.

“Sasa nimepata picha kwa nini mahali hapa panaitwa mzimu tete.Ni kwa sababu ya mambo haya yaliyokuwa yanafanyika.Watu walikuwa wanauliwa na kuja kutupwa huku.” Alisema Mathew

“Sikufahamu uwepo wa jambo kama hili.Mimi

nimefika huku mara moja tu” alisema Faraji.

“Naanza kuhisi kama vile SNSA imepoteza mwelekeo na inafanya mambo tofauti na malengo ya kuanzishwa kwake.Kuna mengi ambayo tunahitaji kuyafahamu kutoka kwako kuhusiana na idara hii” alisema Mathew na kuufunika mfuniko ule wakatoka ndani ya kile chumba.Faraji aliendelea kutiririkwa jasho.

Ilimchukua Ruby Saa mbili kufanikisha kile kilichowapeleka mahali pale.

“Kila kitu tayari” alisema Ruby aliyekuwa amechafuka vumbi lililokuwamo ndani ya kile chumba.

“Ruby mahali hapa hatutarudi tena labda kwa sababu nzito.Umeshuhudia changamoto iliyopo kufika mahali hapa hivyo nataka kabla hatujatoka humu ujiridhishe kuwa kila kitu kiko sawa sawa” alisema Mathew.Ruby aliyekuwa anapakia vifaa vyake katika begi hakusumbuka kumtazama Mathew,alijibu kwa ufupi.

“We’re in”

Walijitahidi kuhakikisha hawaachi alama yoyote inayoweza kuashiria uwepo wao mahali pale kisha wakafunga nyumba ile vizuri kama ilivyokuwa wakaondoka mahali pale.

****

Tayari kulianza kupambazuka Mathew na Ruby waliporejea katika makazi yao ya muda.Walipotoka mzimu tete

walimrudisha kwanza Faraji nyumbani kwa Gavana alikoacha gari lake.

Hakukuwa na muda wa kupoteza,Ruby aliingia katika ofisi yao akaweka mambo sawa kazi iliyomchukua dakika zaidi ya kumi.Mathew ambaye mavazi yake hayakuwa yanatazamika kutokana na kuchafuka, alisimama pembeni akimtazama Ruby kwa makini sana.Aliomba kimya kimya kila kitu kikubali kwani kurudi tena kule walikotoka ni shughuli nzito.

Baada ya Ruby kuunganisha vifaa vyake alimuonesha Mathew dole gumba ishara kuwa mambo yako vizuri.Mathew alitabasamu akamfuata

“Nilikuwa ninaomba kimya kimya ili mambo yasikatae” alisema Mathew

“Toka lini umeacha kumuamini Ruby? Katika idara yangu nikikwambia kitu niamini” alisema Ruby.

“Sasa kazi inaanza rasmi.” Alisema Mathew

“Tunaanzia wapi? Aliuliza Ruby

“Tunaanza kwa kuwachunguza viongozi wa chama cha ukombozi wa Afrika.Regina alituambia kwamba Amani ambaye aliuawa alikuwa anamchunguza mwenyekiti wa chama cha ukombozi.Tunaanza na sisi kumchunguza mwenyekiti huyo.Tutawachunguza pia viongozi wengine wa juu wa chama hicho ambao wanazifahamu siri za chama.Hatutasahau

kumchunguza pia mgombea wao wa uraisi kumfahamu ni nani.Wakati huo huo tutajielekeza pia katika kumtafuta Gosu Gosu na ili tujue mahali alipo Gosu Gosu tutalazimika kujua kwanza mahali alipo Ambola.Mwanamke yule kuna kitu anakifahamu kuhusu suala la Gosu Gosu" alisema Mathew na kuinuka akaenda kumchukua Regina.

"Regina nimekuleta hapa kuna mambo tunahitaji utusaidie .Leo tunaianza rasmi kazi yetu ya uchunguzi kubaini

mipango ya hujuma katika uchaguzi mkuu.Ulituambia Amani alikuwa anamchunguza mwenyekiti wenu lakini kwa bahati mbaya aliuawa kabla ya kukupa kile alichokipata katika uchunguzi wake.Tunaanza kumchunguza huyo mwenyekiti wa chama.Tunaomba kumfahamu jina lake,namba yake ya simu kama unaikumbuka,aina ya gari analoendesha,kinywaji anachotumia,rangi anayoipenda.Hali yake ya ndoa nikimanisha ana mke na watoto wangapi? Wako wapi?

Ana kimada? Tunataka kufahamu mambo kama hayo.” Alisema Mathew.

“Inaonesha hamjalala usiku wa leo” alisema Regina

“Tutalala pale tutakapohakikisha nchi ni salama.Tusipoteze muda tafadhali tupe taarifa” alisema Mathew.

“Mwenyekiti wa chama cha ukombozi wa Afrika anaitwa Israel Maungwana.Umri sifahamu ana miaka mingapi.Namba yake ya simu sijaiweka

kichwani.Kwa ufupi tu ni kwamba mimi si mtu wa karibu sana na mwenyekiti huyo wa chama.Mahusiano yetu ni ya kikazi.Makutano yetu ni katika vikao vya kazi hivyo sijapata wasaa wa kufahamu mambo yake mengi.” Alisema Regina

Wakati Regina akitoa maelezo yake,Ruby alikuwa anaandika haraka haraka katika kompyuta yake na mara Regina akaiona picha katika runinga iliyokuwa ukutani.

“That’s him.Yule ndiye mwenyekiti wa chama” alisema Regina.Mathew aliinuka akaisogelea runinga ili aitazame vizuri ile picha.

“I know this guy.” Alisema Mathew

“You know him? Aliuliza ruby

“Yes.I know him” alijibu Mathew na kumgeukia Regina.

“Una hakika huyu ndiye mwenyekiti wa chama? Aliuliza Mathew.

“Ndiyo.Huyu ndiye Israel Maungwana mwenyekiti wa chama cha Ukombozi wa Afrika” alisema Regina.

“Mathew umeshtuka baada ya kumuona huyu mtu.Who is he? Aliuliza Ruby.Bado Mathew alikuwa amesimama akiitazama ile picha runingani.

“Mathew ! aliita Ruby.

“Ni nani huyu mtu? Aliuliza Ruby”

“Jina lake siyo Israel Maungwana.This man is very

very dangerous .” Alisema Mathew akiwa bado amesimama akiitazama ile picha ya mwenyekiti.

“Hapa kuna kazi kubwa.Huyu mtu ni hatari mno zaidi ya mnavyofikiria” alisema tena Mathew.

“Tuambie tafadhali ni nani huyu mtu? Aliuliza Ruby

Mathew alienda kuketi katika kiti.Bado aliendelea kuitazama ile picha halafu akavuta pumzi ndefu.

“Toka nimemfahamu Mathew Mulumbi ni mara ya kwanza ninamuona akiitazama picha ya mtu namna hii.Ni mara kwanza amerudia mara mbili kutamka kuwa mtu huyu ni hatari.Ni mara ya kwanza Mathew ameonesha hofu.Haijawahi kutokea hata mara moja.Huyu mtu lazima ni hatari zaidi ya ziraili mtoa roho” aliwaza Ruby.

NI NANI ISRAEL MAUNGWANA? KWA NINI MATHEW AMEINGIWA HOFU BAADA YA KUMUONA? AMBOLA YUKO WAPI? MIPANGO YA GOSU GOSU ITAFANIKIWA?

NDUGU MSOMAJI ENDELEA KUFUATILIA SIMULIZI HII